
SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa


**Ukatili unaowasibu watoto wanaobadili petroli kuwa bangi**
UKURASA 4



**MAISHA** Jumapili
Desemba 19, 2021 Nipashe
Baba, Mama na Mwana



X-mas na nyama choma



**NYUMBA:** Namna ya kupamba nyumba yako msimu huu wa sikukuu



KATUNI

NGOZI KAVU
**Tatizo la wengi**




# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
Jumapili Desemba 19, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0580799
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Polepole, Gwajima wawekwa kiporo

**Ripoti** mbili dhidi yao zajadiliwa Kamati Kuu... *Endelea ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM ambaye pia ni Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, nje ya Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma baada ya kumalizika kwa Kikao cha Kawaida cha Halmashauri Kuu ya Taifa jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali yatoa ufafanuzi ongezeko wenye mafua

UKURASA 2

## Watumishi waliong'ang'ania mjini wapewa wiki 2 kuhama

UKURASA 5

MICHEZO YANGA YAJIPANGA KUENDELEZA DOZI UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

# Jafo aonya ukataji miti

**Na Mwandishi Wetu,** SONGEA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amewataka wananchi kuendelea kutunza vyanzo vya maji kwa kuepuka ukataji miti ovyo hasa maeneo ya milimani.

Dk. Jafo alitoa wito huo jana alipotembelea na kukagua hifadhi ya misitu na chanzo cha maji katika milima ya Matogoro wilayani Songea mkoani Ruvuma wakati wa ziara yake ya kikazi.

Katika ziara hiyo, waziri huyo alionyesha kuridhishwa na usimamizi wa misitu iliyopo katika eneo hilo ambalo maji yake hutumika kutoa huduma kwa wananchi wa Manispaa ya Songea kupitia Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (SOUWASA).

"Ndugu zangu, haya maji yanatiririka kwa sababu ya utunzaji wa misitu hii na mimi ninaamini inawezekana katika maeneo mengine, uharibifu wa mazingira umeshaanza na inawezekana uharibifu wa maji ungekuwa haujatokea, tungekutana na maji yanafurika.

"Hatuwezi kupata haya maji kama uharibifu wa mazingira ungekuwa mkubwa. Kwa mfano leo hii hawa watu wangeamua kufyeka misitu yote kwa ajili ya mkaa au kuni, hiki chanzo maana yake kitakuwa ni ghost project (mradi hewa).

"Yaani kutakuwa hakuna maji yoyote yanayotiririka, maana yake kama Songea kuna upungufu wa lita za maji milioni sita kwa siku ambapo vyanzo vya maji ni hii milima ya Matogoro, hali ya Mji wa Songea itakuwa ni mbaya sana," alionya.

Waziri huyo aliwataka wananchi kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti kwa wingi hususani kwenye vyanzo vya maji na kuitunza ili kuepusha uhaba wa maji.

Alitoa rai kwa viongozi wa mikoa, wilaya na Wakala Misitu Tanzania (TFS) kuhakikisha wanachukua hatua za kisheria dhidi ya yeyote anayefanya shughuli inayohatarisha usalama wa vyanzo vya maji na mazingira.

Waziri Jafo pia alitembelea na kukagua mazingira katika machinjio ya kisasa yaliyoko Manispaa ya Songea, alikoonyesha kuridhishwa na usimamizi wa mazingira.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa (kulia) akishiriki shughuli za ujenzi wa karo kwenye Zahanati ya Nyabilezi iliyojengwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa miradi ya mfuko huo wilayani Chato, mkoani Geita. Anayeshirikiana naye ni Mbunge wa Jimbo la Chato, Medard Kalemani. **PICHA: JAMES MWANAMYOTO**

# Polepole na Gwajima wawekwa kiporo CCM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HATMA ya wabunge Humphrey Polepole, Jerry Silaa na Askofu Josephat Gwajima iko mikononi mwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa baada ya taarifa ya Kamati ya Maadili ya Wabunge kutua mbele ya kamati hiyo.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipotoa taarifa ya kikao cha Halmashauri Kuu ya chama hicho kwa waandishi wa habari.

Shaka alisema wabunge hao watatu wataitwa kwenye Kamati Kuu ya chama hicho ili kupatiwa haki yao ya msingi na kikatiba ya kusikilizwa.

"Tayari taarifa ya Kamati ya Maadili ya Wabunge wa CCM na ile ya bunge ipo Kamati Kuu na wabunge hawa watatu wataitwa ili kupatiwa haki yao ya msingi ya kujieleza katika siku ambayo itapangwa na Kamati Kuu," alisema Shaka. Mbunge wa Kawe, Gwajima, Mbunge wa Ukonga, Silaa na Mbunge wa Kuteuliwa, Polepole, hivi karibuni wametuhumiwa kuwa na mienendo ya kitabia isiyofaa ndani ya chama hicho.

Akizungumzia mambo mengine yaliyojadiliwa katika kikao hicho, Shaka alisema hoja kuu zilikuwa ni pamoja na kutoa pongezi kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya katika kusimamia utekelezaji wa ilani ya chama.

"Rais anasimamia ilani katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Rais Samia ameweza kutatua kero na changomto za wananchi katika masuala ya huduma za maji, afya na umeme," alisema.

Shaka alisema kuwa kisiasa, Rais yuko tayari kuunganisha nchi na kwa kulithibitisha hilo hivi karibuni alishiriki mkutano wa wadau wa masuala ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini.

Katibu huyo pia alizungumzia maandalizi ya maadhimisho ya miaka 45 ya kuzaliwa kwa CCM yatakayofanyika Februari mwakani, akisema chama hicho kimerudisha utaratibu wa zamani wa maadhimisho ya kitaifa ambapo uzinduzi utafanyika Kusini Unguja Januari 19, 2022 na kilele chake ni Februari 5 mwakani mkoani Mara.

"Maadhimisho hayo ya kuzaliwa kwa CCM yataambatana na shughuli mbalimbali ikiwamo matembezi ya mshikamano na kutafakari uchaguzi wa ndani ya chama ambao unatarajiwa kufanyika mwakani pamoja na kutafakari Azimio la Arusha linalosisitiza uongozi bora na siasa safi," alisema.

Shaka alisema chama kinatoa shukrani kwa wanachama wake kwa kuwa pamoja katika kuwaunga mkono viongozi wakuu wa chama.

# Serikali yatoa ufafanuzi ongezeko wenye mafua

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imekiri taarifa za kuwapo kwa ongezeko la watu wenye dalili za mafua, kukohoa, maumivu ya mwili na kuchoka, ikifafanua kuwa hiyo ni hali ya kawaida ambayo hutokea kila mwaka (seasonal influenza) na huchangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, Wizara ya Afya na taasisi zake wanaendelea kufuatilia kwa karibu viashiria vya mwenendo wa hali hiyo.

"Wizara inashauri wananchi wenye dalili hizi za kukohoa, mafua, maumivu ya mwili na kuchoka watoe taarifa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili wafanyiwe uchunguzi wa kitaalamu na wapatiwe matibabu stahiki," alisema Dk Sichalwe katika taarifa yake hiyo.

Aliongeza kuwa pamoja na hali hiyo ya mwenendo wa mafua ya kawaida, wizara inaendelea kukumbusha na kutoa tahadhari kwa kila mtu kuendelea kuchukua hatua zote muhimu za kujikinga na janga la UVIKO-19.

Alishauri kuwa watu wanapaswa kuepuka misongamano isiyokuwa ya lazima, kunawa mikono, kuvaa barakoa na kuhakikisha kuwa kila mtu anapata dozi kamili ya chanjo.

Alisema wizara imeelekeza Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), vyuo vikuu na wataalamu wa afya kuendelea kutoa takwimu na elimu kutokana na utafiti wa kisayansi ambao wamekuwa wakifanya kuhusiana na visa vya mafua, ili kuhakikisha umma unaendelea kupata taarifa za mwenendo wa mafua nchini.

"Ninapenda kuwakumbusha wananchi kuwa ugonjwa wa UVIKO-19 bado upo na huenda maambukizi ya ugonjwa huu yakaongezeka hasa tunapoelekea mwisho wa mwaka unaohusisha kipindi cha msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

"Hivyo, ni vyema tuzingatie kuchukua tahadhari zote kama zinavyoelimishwa na wataalamu wa afya bila kusahau kuchanja, pia tunatoa wito kwa wananchi kutoa taarifa za tetesi za viashiria vya magonjwa ya mlipuko kutoka katika jamii kupitia namba ya simu 199 bila malipo," alisema Dk. Sichalwe.

Jana mchana Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) lilitangaza kuahirisha mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Kagera Sugar na Simba baada ya kupewa taarifa kwamba wachezaji wengi wa timu ngeni walikuwa na dalili hizo za mafua hayo ya msimu na kukohoa.

# HABARI KITAIFA

## Mwigulu avihimiza vyuo kufanya utafiti

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Lameck Nchemba amewaagiza watendaji na watalaamu wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) kuongeza bidii katika kufanya utafiti utakaochangia kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa nchi.

Agizo hilo liliwasilishwa jana na Mhasibu Mkuu wa Serikali, Leonard Mkude kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Nchemba, katika mahafali ya 35 ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na ya tisa kwa upande wa Kanda ya Ziwa yaliyofanyika mkoani Mwanza.

Mkude alisema ni jambo la kufurahisha na kutia moyo kuona chuo kinatekeleza kwa vitendo moja ya majukumu yake ya msingi ya kutoa huduma ya ushauri elekezi kwa jamii, halmashauri na taasisi mbalimbali.

"Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea kuunga mkono juhudi za ujenzi wa Chuo cha Mipango kwa kuendelea kutoa fedha za maendeleo na kuweka msukumo ili kiendelee kujenga majengo ya kisasa yanayokidhi mahitaji," alisema.

Mkude alifafanua kuwa katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru, nchi imepiga hatua kubwa ya maendeleo katika nyanja ya elimu, ikiwamo ongezeko kubwa la shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vya elimu ya juu na serikali itaendelea kujenga vyuo vya ufundi katika kila mkoa ili kutoa fursa kwa vijana wanaomaliza elimu ya sekondari na msingi kupata ujuzi.

Aliupongeza uongozi wa chuo hicho kwa kuwekeza katika ushirikiano na wadau wa maendeleo wakiwamo UNDP, FAO, UNICEF, NUFFIC, EU, AGRA na wengine katika mapambano dhidi ya ujinga, maradhi na umaskini pamoja na kuwezesha kutoa huduma ya ushauri elekezi kwa jamii.

Aliwataka wahitimu kutumia ujuzi, elimu na maarifa waliyoyapata chuoni hapo kwa manufaa ya umma kwa kuanzisha vikundi vya uzalishaji mali kwa kutumia fursa ya mikopo nafuu inayopatikana katika halmashauri nchini.

Pia alitoa wito kwa waajiri na wadau wote wa maendeleo nchini kuwatumia vijana hao ambao wameiva na kubobea katika fani ya mipango ya maendeleo ambayo ni muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote duniani.

Mkuu wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP), Prof. Hozen Mayaya, aliishukuru serikali kwa jinsi inavyotenga fedha za maendeleo zinazosaidia kujenga majengo ya chuo hicho katika eneo la Kitumba A, kata ya Kisesa wilayani Magu ambako mahafali ya mwaka huu yamefanyika huko kwa mara ya kwanza.

Alisema kituo cha mafunzo Kanda ya Ziwa Mwanza kimekuwa na ongezeko la udahili kila mwaka sambamba na ongezeko la wahitimu ambapo mahafali ya kwanza ya mwaka 2011/12 yalikuwa na jumla ya wahitimu 269, ilihali mwaka huu kuna jumla ya wahitimu 2,718.

"Ili kuongeza wigo wa fursa za ajira miongoni mwa wahitimu wetu, chuo kimeanzisha kituo cha ubunifu na ujasiriamali, ambapo wanafunzi wanapata nafasi ya kujifunza masuala ya ubunifu na ujasiriamali, hivyo kuwa tayari kuajiriwa na kujiajiri," alisema Prof. Mayaya.

# 'Kigogo' CWT ataka uaminifu kwa walimu

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

KATIBU Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Deus Seif, amewataka walimu kuwa waaminifu ili kurejesha imani na hadhi ya kada hiyo kwa wananchi na serikali.

Mbali na kutaka walimu kuwa waaminifu, Seif pia amesema siri ya mafanikio ya sasa ya Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, na Waziri wa Madini, Dotto Biteko, ni uwajibikaji mzuri na uadilifu wao wakati wakitumikia nchi katika ngazi mbalimbali za ualimu.

Seif alitoa kauli hiyo jana mkoani Mtwara aliposhiriki hafla ya kuwakabidhi zawadi walimu, wanafunzi na shule zilizofanya vizuri katika mitihani mbalimbali ya kitaifa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. Alisema kuwa kabla ya kuingia katika siasa, Majaliwa aliwahi kuwa Katibu wa CWT Wilaya ya Mtwara na kujitolea kujenga ofisi ya chama hicho, jambo alilolifanya pia alipohamishiwa mkoani Singida.

"Waziri Mkuu Majaliwa na Dotto Biteko, wakiwa katika nafasi hizi hizi za ualimu waliacha alama katika maeneo yao waliyopangiwa kazi na Mwenyezi Mungu akawabariki, leo ni viongozi wakubwa nchini.

"Na hii yote ni kwa sababu ya uaminifu na uwajibikaji wao kwa ajili ya taifa, hivyo kila mmoja wetu atekeleze wajibu wake kwani kesho yetu hatuijui" alisema Seif. Alitumia sherehe hizo kuwaonya watumishi wa umma wasiowatendea haki walimu, akisisitiza kuwa yeyote atakayecheza na kada hiyo, ni wazi anajichimbia kaburi la kusahaulika katika historia ya waadilifu wa nchi. Alisema ili walimu wafundishe na kuifurahia kazi yao, ni muhimu mwongozo wa elimu ukafuatwa ikiwa ni pamoja na kupata mishahara ya kuridhisha na kwa wakati, kuwa na idadi ya wanafunzi wanaotakiwa katika kila darasa, kupandishwa madaraja kwa wakati na motisha.

Kuhusu uaminifu kwa walimu, Seif alisema ni aibu kuona kaktika miaka ya karibuni mitihadi ya kitaifa ya madarasa tofauti kusimamiwa na vyombo vya dola kwa kuwa tu baadhi ya walimu wameshindwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo.

"Ninawaambia mitihani mnayoona inalindwa na askari wakiwa na mitutu ya bunduki haina tatizo lolote, tatizo lipo kwetu walimu tumeshindwa kuwasaidia wanafunzi, sasa tunategemea tufanye ujanjaujanja kuonekana tumefaulisha vizuri, lakini nawaambieni hili linaua maarifa ya watoto wetu," alisema Seif.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, akizungumza katika sherehe hizo, alisema serikali imedhamiria kuboresha mazingira ya walimu kufundishia kwa kuanza na maboresho ya madarasa mapya na shikizi yaliyojengwa kupitia fedha zilizotolewa na serikali kupitia kutokana na mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mtwara, Adam Shemnga, alisema dhamira ya halmashauri hiyo ni kushika nafasi ya kwanza kimkoa katika mitihani ijayo kutoka nafasi ya nne iliyoshika mwaka huu.

Alisema shule zote zilizofanya vizuri zimezidi wastani wa ufaulu wa kitaifa kwa kupata asilimia zaidi ya 83 huku malengo ya kitaifa ikiwa ni ufaulu wa asilimia 82.



Mhasibu Mkuu wa Serikali CPA, Leonard Mkude, akimtunuku cheti mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili, Daudi Joseph, katika mahafali ya 35 ya Chuo cha Maendeleo ya Vijijini na ya tisa katika Kanda ya Ziwa, jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbarawa akoshwa ujenzi wa SGR Kanda ya Ziwa

**Na Mwandishi Wetu, MWANZA**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Isaka - Mwanza chenye urefu wa kilometa 341 unaendelea kwa kasi.

Prof. Mbarawa pia amesema serikali imekwishalipa malipo ya awali kiasi cha Sh. bilioni 376.36 kwa mkandarasi kwa ajili ya kuanza kazi za awali ikiwamo ujenzi wa tuta la reli na hadi kufikia hatua hiyo mradi unaendelea vizuri na serikali haidaiwi.

Aliyasema hayo jijini Mwanza jana alipokagua maendeleo ya mradi huo unaotekelezwa kwa muda wa miezi 36 kwa gharama ya Sh. trilioni 3.062 na kampuni ya China Civil Engineering Construction (CCEC) na China Railway Construction Corporation (CRCC).

"Kazi zinaendelea, mkandarasi amejipanga vizuri na tunategemea atakamilisha ujenzi huu kwa wakati kama ulivyopanga,"

Prof. Mbarawa alisema. Prof. Mbarawa aliipongeza jitihada zinazofanywa na serikali kuhajkikisha fedha za miradi zinaendelea kutolewa kwa wakati kwa manufaa ya wananchi na kusaidia kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji katika ukanda huo.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alisema ulianza Mei mwaka huu na unatarajiwa kukamilika Mei 2024.

Mkurugenzi huyo alisema mradi huo unahusisha madaraja makubwa 43, vivuko vya chini 44, vya juu 23 na makalvati 591 na daraja refu eneo la kuingia Mwanza, vituo tisa, stesheni kubwa ya Mwanza na pia kutakuwa na karakana kubwa eneo la Fela na Tabora kwa ajili ya reli hiyo.

Kadogosa pia aslisema tayari wamekwishalipa kiasi cha Sh. bilioni 2.8 kwa ajili ya fidia kwa wananchi waliopisha mradi huo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA.**
**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA.**
**Usimamizi wa mirathi 232 /2021.**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU NASSORO Y. NASSORO WA CHANG'OMBE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA YUSSUFU NASSORO YUSSUFU.**

**TANGAZO**
(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 12 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika
**Imetolewa leo tarehe 06 Mwezi 12 Mwaka 2021.**
PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

**RIPOTI MAALUMU**

# Ukatili unaojiri dhidi ya watoto wanaobadili petroli kuwa bangi

**Na Elizabeth Zaya**

NI majira ya saa 12 asubuhi, jua likiashiria mawio, watoto wenye umri wa kuwa shule ya msingi, wanaonekana wakipita katikati ya magari yaliyosimama eneo la Ubungo Mataa mkoani Dar es Salaam, wakiomba msaada kwa abiria wa daladala.

Macho ya watoto hao yanaonekana kama ya mtu aliyelewa, hata namna wanavyotembea, ni ishara tosha kwamba kuna kilevi wametumia. Macho yao yamelegea mithili ya mlevi wa pombe au mtumiaji wa dawa za kulevya.

Si hivyo tu, midomo ya baadhi yao inaonekana kuwa na unyevunyevu unaofanana na mate na pua zao zinaonekana kuzidiwa na wingi wa kamasi.

Kingine ambacho Nipashe Jumapili inakibaini na kupatwa na maswali yanaisukuma kufanya udadisi, ni watoto hao kuvaa sweta lenye mikono mirefu ilhali hali ya hewa Dar es Salaam kipindi hiki ni ya joto kali.

Pembeni ya barabara ya Nelson Mandela, jirani na makutano ya barabara nne eneo la Ubungo, anaonekana mmoja wa watoto hao akinunua vitumbua na chai kwa mfanyabishara mdogo wa chakula na hapo ndipo Nipashe inapata nafasi ya kupata undani wa madhila yanayowakabili watoto hao.

"Nina miezi mitatu sasa tangu nianze kufanya kazi hii ya kuomba. Ninaishi hapa kwa sababu ndugu yangu ninayemtegemea, ambaye alinitoa kwetu Mbeya kuja hapa Dar (es Salaam) alikamatwa na polisi," anasimulia mtoto aliyejitambulisha kwa jina la Jafari.

Mtoto huyo (9) anaendelea na simulizi yake, akitamka: "Kaka yangu ndiye alikuwa ananilea, alinitoa Mbeya, lakini alikamatwa na kupelekwa polisi, nikabaki napata shida ndiyo nikawa natembea kila sehemu kuomba chakula hadi nikafika hapa Ubungo.

"Sehemu ya kulala yenyewe ni ya shida, tunaruka uzio uliowekwa chini ya daraja la juu ndio tunalala humo. Humo tunamolala askari wanatufukuza, huwa tunajificha sana."

Mtoto huyo anadai kuwa katika eneo hilo la Ubungo, kuna watoto zaidi ya 50 ambao wanaishi maisha hayo ya kuomba na wengi wao wametoka mikoa mbalimbali kwa kuletwa na ndugu zao kisha kutelekezwa.

Katika udadisi wake kupitia ushuhuda wa mtoto huyo, Nipashe Jumapili inabaini watoto wengi walio katika eneo hilo, wameshajiingiza kwenye uvutaji kilevi wanachokitengeneza kwa kuchanganya mafuta ya petroli na gundi inayotumika kwenye viatu.



Watoto wakitumia chupa iliyowekwa petroli ambayo huitumia kwa kunusa kupata ulevi.

"Ukiwaona watoto wengi hapa utaona wako kama mateja, wanavuta gundi wanaiweka kwenye chupa ya plastiki halafu wanaificha kwenye sweta mkononi, halafu wanavuta, ila mimi sivuti.

"Sivuti kwa sababu wanaovuta wanalegea na wanasinzia tu ovyo, wanasema hiyo inawasaidia kuwaondolea aibu wanapoomba kwenye gari na wengine wakilewa hivyo wanalala mchana ili usiku ndiyo waanze kuomba na wasilale kwa sababu wanaogopa kubakwa na yale mabaunsa 'yanayotukimbizaga' usiku.

"Kuna wenzetu (watoto) wamekubali yaishe, wame... (alitamka neno lenye dhana ya kufanyiwa ukatili), wanatembea kama wana ulemavu, utawaona tu wapo wengi hapa," anasema mtoto huyo.

Wakati mazungumzo na Jaffari yakiendelea, linatokea kundi la wenzake 10 baadhi yao wakiwa wameshika chupa za plastiki zikiwa zimechomekwa mirija ndani, huku wakitamka maneno yaliyokosa tafsida, wakitaka huduma ya chakula kwa 'mama ntilie'.

Mmoja wa watoto hao, Kizito (jina la pili tunalihifadhi) anasema wamejifunza kuvuta kilevi hicho baada ya kupata darasa kutoka kwa mwenzao na wanaona kinawasaidia kupata usingizi na kuwaondolea aibu katika kazi yao hiyo ya kuomba.

"Yaani ukipiga hii dada yangu (mwandishi), dunia unaiona raha sana na unapiga kazi balaa, hakuna cha aibu wala kumwogopa mtu. Hata wewe ukijaribu utaipenda na hutatamani kuacha," adai Kizito huku akisogeza chupa yenye kilevi hicho kwenye mdomo wa mwandishi.

Kizito anabainisha wananunua gundi Manzese na mafuta ya petroli huyanunua kwenye vituo vya mafuta, akifafanua uzoefu wao kwamba lita moja inatumika kwa kundi lao la Ubungo kwa siku mbili, kila mmoja akichangia ununuzi huo.

"Petroli tunanunua sheli kwenye kichupa cha maji ya kunywa (anaonyesha chupa), tunajichangisha pesa, lakini gundi huwa tunapata kwa mtu mmoja eneo la Manzese, anajulikana sana kwa jina la bibi. Kichupa kidogo kama hiki cha juisi (anaonyesha) anatuuzia Sh. 1,000," alisema.

**USHUHUDA MAMA NTILIE**

Peter Lucas, fundi viatu eneo la Ubungo, anasema kumekuwa na ongezeko la idadi ya watoto kwenye eneo hilo na wanapowahoji, wanadai wametelekezwa na watu waliowatoa mikoani kuwaleta Dar es Salaam.

"Niko hapa muda mrefu sasa nikifanya kazi hii ya kushona viatu. Kila siku sasa idadi ya watoto inaongezeka, matokeo yake vitu wanavyofanya na kufanyiwa hapa ni vya hatari.

"Wengine kama unavyoona ni watoto wadogo lakini wameshakuwa mateja kwa kuvuta hiyo gundi wanayochanganya na petroli, kwenye hizo chupa zao ndimo wanamoweka, tumekuwa tukiwanyang`anya ukiwaona wanavuta ndiyo maana unaona wanaficha, lakini hawasikii.

"Kibaya zaidi wakishalewa hivyo, wakienda kuomba kule kwa wenye magari yao, watu wazima wengine wasio na hofu ya Mungu wanawabeba kwenye magari yao kuondoka nao na wakirudi hapa unaona wanachechemea tu. Ukimuuliza anakwambia kaharibiwa.

"Na hivi karibuni kuna watoto kama watatu hivi tuliwaonea huruma tukawapeleka hapo Hospitali ya Sinza Palestina, walikuwa wameharibika wanapepesuka, wanajidondokea tu," alisema.

Fundi Lucas anaishauri serikali kuwasaidia watoto hao kwa kuwaondoa katika eneo hilo ili wasiharibu watoto wengine.

Mama ntilie katika eneo hilo, Mariam Hamis, anasema anapata wakati mgumu kuwauzia chakula watoto hao kwa kuwa wanakuwa wamelewa kiasi cha baadhi yao kutokwa na udenda mdomoni, hivyo anaingiwa hofu ya kupoteza wateja wake.

"Unakuta mtoto anakuja hapa amechafuka, anapepesuka na anatoa udenda mdomoni na ameshika hizo dawa wanazovuta mkononi. Kwa hiyo mpaka unaona ukimpatia chakula kwenye sahani wanazotumia wateja wengine wa kawaida unaona utawapoteza.

"Nimelazimika kutafuta vyombo maalumu kwa ajili yao tu, na wateja wangu wanalijua hilo. Lakini mimi ni mama, huwa nawaonea huruma, nawapatia chakula na kipimo chao huwa ni tofauti, huwa wananunua cha Sh. 1,000 badala ya Sh. 1,500 .

"Wakati mwingine anakuja hapa anakwambia hana pesa na ana njaa, umkopeshe, inabidi umpe tu, akipata analeta na ni waaminifu sana. Inabidi serikali iwaondoe, la sivyo watazidi kuvuta wengine na kuwaharibu zaidi," Mariam anashauri.

Katika ufuatiliaji wake, Nipashe Jumapili pia ilibaini watoto wengine waliotumbukia kwenye matumizi ya kilevi hicho wako kwenye Kituo cha Mabasi cha Magufuli.

Bibi anayeuza gundi inayotumiwa na watoto hao (jina tunalo), anaiambia Nipashe Jumapili eneo la Manzese kuwa ana wateja wengi na huwa hafuatilii wala kuwahoji matumizi yake kwa wateja wake.

Daktari wa Binadamu katika Hospitali ya Sinza Palestina, Dk. Gloria Lema, anayetoa huduma kwenye kitengo maalumu kinachoshughulikia watoto waliofanyiwa ukatili na walioathirika na dawa za kulevya, anakiri wamekuwa wakipokea watoto waliothiriwa na dawa za kulevya.

"Tumepokea baadhi ya watoto ambao wanavuta kilevi wanachochanganya petroli na gundi. Baada ya kupokea wengi wa namna hii ilibidi tufuatilie na ndipo tukabaini kwamba wanalazimika kutumia kilevi hiki baada ya serikali kufanya kazi ya ziada ya kudhibiti dawa hizi zingine za kulevya, kwa hiyo wengi wamegeukia kwenye aina hiyo ya ulevi.

"Gundi na petroli ni kilevi kingine kibaya kama ilivyo kwa bangi au dawa zingine za kulevya na zinaathiri mambo mengi mwilini ikiwamo afya ya akili na ndiyo maana mtu anayetumia aina hii lazima muda wote anaishiwa nguvu na anakuwa anasinzia. Akizoea kutumia lazima awe na uraibu na kupona kwake akiamua kuacha inachukua muda mrefu kidogo," Dk. Gloria anasema.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Dar es Salaam, Judith Kimaro, anasema wana taarifa ya watoto hao na wamekuwa wakiwasaidia kuwapeleka kwenye vituo vya kusaidia walioathiriwa na dawa za kulevya.

Pili Missana, mmiliki wa kituo cha kusaidia walioathirika na dawa za kulevya kilichoko Kigamboni, Dar es Salaam, anasema kwa mwezi amekuwa akipokea wastani wa watoto 10 wanaovuta gundi iliyochanganywa na petroli na kuwakabidhi kwa maofisa ustawi wa jamii.

**KAMISHNA KUSAYA**

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Gerald Kusaya, anasema gundi, petroli, shisha havijajumuishwa katika Sheria Na. 5 ya Mwaka 2015 ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya.

"Mimi mwenyewe nimekutana na hao watoto wanaovuta hiyo gundi, na siyo siri wameharibika, lakini kwa bahati mbaya sheria inayotuongoza haijajumuisha hivyo vitu, la sivyo wadau wakae tena na kujadili kupeleka sheria bungeni ili ifanyiwe marekebisho," anasema.

Anasema watoto wanaovuta dawa za kulevya nchini wapo na baadhi yao wako kwenye vituo ambavyo vimetengwa na serikali kwa ajili ya kuwapatia dawa waathirika wa dawa hizo.

"Na kuna mmoja nilimkuta kwenye kituo chetu mkoani Tanga, ana miaka 16 na nilipozungumza naye anashindwa hata kuongea vizuri, anasema alianza kutumia dawa tangu akiwa darasa la tano, na tunapokea taarifa pia kutoka shule mbalimbali za sekondari na msingi kuhusiana na watoto wanaovuta dawa hizo," anasema.

Kusaya anabainisha kuwa takwimu walizonazo kwa sasa zinaonyesha zaidi ya watu 500,000 nchi nzima wanatumia dawa za kulevya na wengi wao wakiwa ni vijana wenye umri wa kuanzia miaka 16 hadi 45.

Haki za watoto zinalindwa katika mikataba mikubwa miwili ya kimataifa ukiwamo wa Haki za Mtoto (CRC) wa mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) wa mwaka 1990, yote ikiwa imeridhiwa na Tanzania.

Vilevile, Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inaelekeza wajibu wa serikali, wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuwalinda watoto.

# HABARI KITAIFA

## Wafanyabiashara wataka mfumo wa Franchising

**Na Romana Mallya**

WAFANYABIASHARA wazawa wameshauri kutumika kwa mfumo wa Franchising ambao utawawezesha kupata wawekezaji watakaowekeza katika biashara zao na kuzipanua kwa haraka katika masoko ya kimataifa.

Dhana ya mfumo wa Franchising unavyojiendesha ni kwamba badala ya mmiliki wa biashara kufungua matawi mwenyewe na kuyaendesha, mwekezaji anakuwa mtu tofauti kwa kuwezeshwa na mmiliki akitumia mfumo mzima wa biashara wa mmiliki.

Kiongozi Mwelekezi wa Mradi wa Africa Franchising Accelerator (AFRAP) ulio chini ya Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Wambugu Gichohi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mafunzo ya waandishi wa habari kuhusiana na mradi huo.

"Mradi huu umefadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kuwawezesha wafanyabiashara wazawa kukuza biashara zao wafikie malengo makubwa kama masoko ya Afrika kama vile wenzetu walivyofanya kukuza biashara zao," alisema.

Gichohi alisema ni vigumu biashara ya Tanzania kufikia masoko nje endapo wataendelea kutumia mifumo ya kawaida iliyozoeleka.

Alisema faida za mfumo huo ni kuwawezesha wafanyabiashara kupata wawekezaji ambao watawekeza kwenye biashara yako na kuipanua kwa haraka zaidi.

"Wawekezaji hawa wanawekeza fedha zao kwenye mradi mtakaokubaliana usiozidi miaka saba halafu wanatoka wakikuachia biashara yako ikiwa ni kubwa.

"Faida nyingine ni ukishaingiza biashara yako kwenye mfumo huu, zile biashara ndogo zitajiendesha kupitia mfumo wako, wenyewe ndio wanaowekeza kwenye kujenga na kuendesha kwenye maeneo utakayowagawia," alifafanua.

Gichohi alisema hiyo inamsaidia mfanyabiashara kukuza biashara yake kwa njia rahisi bila kutumia fedha nyingi.

Pia alisema kama mfanyabiashara anataka bidhaa zake zipatikane kote duniani kwa sasa ni vigumu kufungua masoko lakini kwa kutumia mfumo huo, utawawezesha wawekezaji wazawa wa nchi husika kuziendesha chini ya makubaliano watakayoafikiana.

Alisema nchi za Afrika Kusini na Misri hazijaanza kutumia mfumo huo kwa sababu uelewa wake upo chini.

"Mradi huu unalenga wafanyabiashara 100 wa Tanzania, tunawaomba waingie kwenye tovuti ya TPSF watakuta 'link' na kujaza fomu ya maombi," alisema.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akisalimiana na wananchi wa Wilaya ya Bunda wakati akiwa katika ziara yake ya kikazi mkoani Mara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waziri ataka hatua kwa watumishi wanaoishi mjini

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amemtaka Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule, kusimamia maelekezo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ya kuhakikisha watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita wanaoishi mjini Geita wanahamia maeneo ya jirani na vituo vyao vya kazi ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mchengerwa alitoa maelekezo hayo jana katika kijiji cha Kakubilo wakati wa ziara yake ya kikazi ya kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma na kukagua utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) mkoani Geita.

Alisema kuwa Waziri Mkuu alikwishatoa maelekezo ya watumishi wote wanaofanya kazi Halmashauri ya Wilaya ya Geita kuishi katika vituo vyao vya kazi lakini bado kuna watumishi wanaishi mjini Geita, jambo ambalo linaathiri utoaji wa huduma kwa wananchi.

"Pamoja na maelekezo aliyoyatoa Waziri Mkuu, nimepata taarifa kuwa kuna watumishi bado wanaishi Geita mjini na sio kwenye vituo vyao vya kazi huku wakitumia gharama za serikali kufikisha kwenye vituo vyao vya kazi kila siku," alisema.

Katika kuhakikisha maelekezo ya Waziri Mkuu yanatekelezwa kikamilifu, Mchengerwa alitoa wiki mbili kwa watumishi wote wa halmashauri hiyo wanaoishi mjini Geita kuhamishia makazi yao kwenye maeneo wanayofanyia kazi.

Mchengerwa alisema kuwa anatarajia ndani ya wiki mbili alizozitoa, watumishi wote wanaoishi mjini watakuwa wamehamia karibu na maeneo wanayotoa huduma kwa wananchi na kwa kuwa ana vyanzo vingi vya kupata taarifa, hatosita kuchukua hatua kwa watakaokaidi.

Alisema yeye ni mlezi wa watumishi wa umma, hivyo amelazimika kwenda wilayani Geita ili kuhakikisha maelekezo ya Waziri Mkuu yanatekelezwa kwa manufaa ya wananchi.

Waziri huyo pia alikagua Zahanati ya Kakubilo iliyojengwa kwa ufadhili wa TASAF na kuwaahidi wananchi wa kijiji hicho kuwa ofisi yake itahakikisha inapeleka watumishi watakaotosheleza kutoa huduma kwa wananchi.

Mchengerwa alihitimisha ziara yake ya kikazi ya siku mbili mkoani Geita kwa kuhimiza watumishi kuishi katika maeneo wanayofanyia kazi ili wawe na tija katika utoaji wa huduma kwa umma.

## Ongezeko la mvua lasababisha mgawo wa maji kupungua

**Na Frank Monyo**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nadhifa Kemikimba, amesema mvua inayoendelea kunyesha katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani imechangia kuongezeka kwa kiasi cha maji katika Bonde la Mto Ruvu na hivyo kupunguza mgawo wa maji.

Alitoa kauli hiyo juzi jijini Dar es Salaam alipofungua mkutano wa wadau wa maji kujadili namna ya kutunza Bonde la Mto Ruvu ambalo ni chanzo kikuu cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam na Pwani.

Alisema kuwa pamoja na mvua inayoendelea kunyesha, pia oparesheni zilizofanywa za kuwaondoa walioingilia mto huo na kuchepusha maji, zimechangia kuongeza maji yanayokwenda Dar es Salaam.

Kabla ya mvua kuanza kunyesha, Bonde la Wami Ruvu walifanya oparesheni ya kuwabaini waliochepusha maji kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji na kumkamata mkulima raia wa China, ambaye alifunga mtambo mkubwa wenye uwezo wa kuvuta maji katika mto huo lita milioni moja kwa saa.

Katika mkutano huo, alisema hali ya maji ilivyo sasa ni tofauti na ilivyokuwa wiki tatu zilizopita hadi kusababisha kutangazwa kwa mgawo na kwamba mgao umepungua kwa kiasi kikubwa na kuna maeneo yalikuwa yanapata maji mara tatu kwa wiki lakini sasa kila siku maji yanapatikana.

"Wiki mbili au tatu kwa kweli maji kulikuwa hakuna, kuna maeneo yalikuwa yanapata maji mara mbili au mara moja kwa wiki, lakini baada ya hii mvua, tulivyoanza oparesheni ya kuwaondoa wale waliochepusha na kuwaondoa wote, ninashukuru Bonde letu la Wami Ruvu walifanya kazi kubwa sana," alisema Kemikimba.

Alisema mvua imesaidia kwa kiasi kuongeza kina cha maji ingawa juhudi zilifanyika hata kabla ya mvua kwa kuwa oparesheni za Bonde la Wami Ruvu zilisaidia kuruhusu maji kutiririka kushuka chini.

Aliongeza kuwa elimu ya matumizi ya maji bado inahitajika kwa kuwa pamoja na maji kuongezeka, bado hawajaruhusu matumizi ya umwagiliaji.

Kaimu Ofisa wa Maji Bonde la Wami Ruvu, Bariki Mmasi, alisema kwa sasa kiasi cha maji kinachopita kwenye kipimo ni lita 10,000 kwa sekunde huku mahitaji yakiwa lita 12,900.

"Kulingana na wadau wetu tuliowapatia vibali vya maji yanayohitajika ni lita 12,900, kwa hiyo kiasi tulichonacho tunaona kwa matumizi ya binadamu tumeanza kuwa vizuri, bado hatujakaa sawa kuruhusu matumizi mengine," alisema Mmasi.

Aliongeza kuwa Bonde la Wami Ruvu bado linaendelea na utaratibu wake wa kutoa elimu mara kwa mara kwa watu wanaofanya shughuli za kibinadamu katika chanzo hicho ili kukitunza, pia kampeni za upandaji wa miti katika kingo za mto huo ili kuutunza na kuuhifadhi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kauli ya Askofu Chilongani kuhusu kazi iungwe mkono

**WIKI** hii Kanisa la Anglikana Tanzania, Dayosisi ya Central Tanganyika (DCT) liliandaa mafunzo ya vikoba na ujasiriamali kwa wanawake wa Ushirika wa Mama wa Kikristo wa Kanisa Anglikana Tanzania (UMAKI).

Mafunzo hayo ya siku tano yalikuwa na lengo la kuwaelimisha zaidi ya washiriki 40 waliohudhuria namna ya kujikwamua kiuchumi kupitia vikundi mbalimbali hususan VICOBA na ujasiriamali.

Wakati wa kufunga mafunzo hayo, Askofu wa DCT, Dk. Dickson Chilongani, aliwahimiza waumini wa kanisa hilo kujishughulisha na uzalishaji mali, ujasiriamali pamoja na kujiunga na VICOBA kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi hatua ambayo itapunguza umaskini na kukuza uchumi kuanzia ngazi ya kaya, kanisa na taifa kwa ujumla. Kimsingi, kiongozi huyo msomi mbobezi katika masuala ya theolojia, alisimama katika nafasi yake kuwakumbusha waumini kwamba jambo la msingi kwa maisha ya binadamu mwenye nguvu ni kufanya kazi.

Suala la kufanya kazi ni la muhimu kwani hata mwanadamu wa kwanza kuumbwa, kwa mujibu wa maandiko matakatifu, baada ya kufukuzwa katika bustani ya Eden, aliambiwa kinagaubaga kwamba atakula kwa jasho lake.

Maana ya kula kwa jasho lake ni kwamba ni lazima afanye kazi ili apata chakula. Pia katika maandiko matakatifu inawekwa bayana kwamba asiyefanya kazi na asile. Kwa mantiki hiyo, kazi ndicho kiini cha mwanadamu katika kupata mafanikio.

Hata katika maisha ya kawaida, kinachomfanya mtu kufanikiwa kwa maana ya kuwa na ukwasi pamoja na mahitaji yote kama vile nyumba, chakula, malazi na mavazi ni juhudi katika kazi. Kwa mantiki hiyo, kila mtu bila kujali itikadi yake kisiasa, imani yake na jinsia, matumizi sahihi ya fursa zinazomzunguka ni kazi na si utegemezi wala kuombaomba na kutegemea misaada.

Kauli ya Askofu Dk. Chilongani imetolewa wakati mwafaka hasa katika kipindi hiki ambacho yameibuka mafundisho mbalimbali, baadhi yakiwapotosha waumini na kuendelea kuwa katika lindi la umaskini. Miongoni mwa mafundisho hayo ni watu kuombewa ili wapate muujiza wa utajiri.


Hatukatai kuombewa lakini jambo la muhimu ni muda wa maombi na ule wa kufanya kazi. Watu hivi sasa wamejenga utamaduni wa kwenda kwenye nyumba za ibada kuanzia alfajiri hadi usiku kwa ajili ya kuombewa na kuonyeshwa ishara mbalimbali za kufanikiwa kimaisha badala ya kufanya kazi kwa ajili ya kujipatia kipato binafsi na kaya kwa ujumla.

Sambamba na hilo, watu wamekuwa wakiaminishwa kupokea muujiza wa kuwa mamilionea, kumiliki mali kama majumba na magari bila kufanya kazi. Mbaya zaidi, wako ambao wamekuwa wakitangaza kufunga siku tatu au saba bila kula kwa ajili ya kuupiga vita umasikini. Matokeo ya yote hayo watu hawa wanaendelea kuwa katika hali walizo nazo au mbaya zaidi.

Watu hao hao wanaosikiliza mafundisho ya namna hiyo, wamekuwa wakiaminishwa kuwa kuombewa wanaweza kupata magari au utajiri lakini unapofika wakati wa viongozi hao (watoa mafundisho) kutaka kupata vitu hivyo wanachangiwa na waumini hao! Ni wakati sasa kwa viongozi wa dini kuhimiza waumini wao namna ya kufanya kazi kwa ajili ya ustawi wao, familia, jamii na taifa kwa ujumla. Ni imani kwamba ndani ya maandiko matakatifu kuna maeneo mengi yanayofundisha umuhimu wa kufanya kazi ili kuwa na maisha bora.

Sambamba na hilo, viongozi wa dini watoe matamko kukemea mafundisho potofu dhidi ya waumini kwamba wanaweza kufanikiwa kwa kupitia miujiza kama ambavyo wamekuwa wakifanya kuhusu maradhi ya corona na ukimwi, rushwa na ufisadi na matendo mabaya yanayofanyika katika jamii kama ukatili dhidi ya kinamama na watoto.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Itapendeza trafiki wakijisahihisha

Na Sabato Kasika

**MARA** kadhaa, Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisikika kwenye vyombo vya habari akiwataka Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani kuwa na lugha nzuri kwa raia na kujiepusha na vitendo vya rushwa.

Rais anasema, baadhi ya askari hao wana vitendo visivyofaa, ikiwamo kusimamisha magari na kuwataka madereva kuwapa fedha, vitendo ambavyo vinakwenda kinyume na maadili ya kazi yao.

Alisema askari anakusimamisha anaingiza kichwa ndani ya gari hajui ndani una nyundo au nondo na akahoji mafunzo gani wanayopata hawa askari.

Rais Samia aliyasema hayo hivi karibuni wakati akifunga mafunzo ya kozi ya uofisa, jijini Dar es Salaam na kukemea vitendo hivyo na kuwataka wafanye kazi yao inavyotakiwa bila kumuonea mtu.

Si mara ya kwanza Rais Samia kukemea vitendo hivyo, kwani kuna wakati aliwahi kukemea na kusema, ana clip zinazoonyesha askari hao wakipokea fedha na kuwataka waache aibu hiyo.

Agosti, mwaka huu, wakati akifungua Kikao Kazi cha Maofisa Wakuu Waandamizi wa Jeshi la Polisi jijini Dar es Salaam, pia alisisitiza kuwa vitendo vya baadhi ya askari kuomba na kupokea rushwa ni aibu.

Kutokana na hali hiyo analiagiza jeshi hilo kukomesha tabia ya baadhi ya askari wake hasa wa usalama barabarani ya kupokea rushwa kwenye magari,na kwamba kufanya hivyo ni kukiuka maadili na kiapo cha kazi yao.

Kwamba kuna video fupi nyingi ambazo zimekuwa zikizunguka ndani na nje ya nchi kupitia mitandao ya kijamii zikionyesha baadhi ya Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani wakiomba na kupokea rushwa kwenye magari.

Nadhani kauli hizo za Rais zingetosha kuwafanya askari hao kujisahihisha na kufanya kazi yao kwa weledi, ili kuepuka madhara ambayo yanaweza kuwakuta baadaye, kutokana na kwamba wameshaonywa mara kadhaa.

> **Wakati huu ambao machinga wanahamishwa, ingependeza kama viongozi wa halmashauri na manispaa wakafanyia kazi malalamiko hayo na kuyapatia ufumbuzi ili kuepusha adha ya kuzunguka na bidhaa zao huku na kule.**

Labda nikumbushe tu kwamba, ukisoma nukuu 10 katika kitabu cha Mwalimu Nyerere cha Tujisahihishe cha mwaka 1962 zipo ambazo Rais ametumia kwa lengo la kuwataka wahusika wabadilike.

Kwa mfano nukuu ya nne inasema; Wengine humwona mwenzao anafanya kosa, badala ya kumwambia pale pale kijamaa kwamba atendalo ni kosa, watanyamaza kimya. Lakini hawanyamazi kimya kabisa.

Mwalimu anafafanua kuwa watakwenda kumteta katika vikundi vya siri. Huku nukuu ya sita ikisema; Ukweli una tabia moja nzuri sana. Haujali mkubwa wala mdogo, haujali adui wala rafiki.Kwake watu wote ni sawa.

Ninaamini kwamba alichokifanya Rais Samia kukemea hadharani vitendo visivyofaa vya baadhi ya Askari wa Usalama Barabarani kinakwenda sawa na nukuu za Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha Tujisahihishe.

Kimsigi, alichosema Rais abiria wanaweza kuwa mashahidi kutokana na jinsi ambavyo wamekuwa wakishuhudia baadhi ya mabasi yakisimamishwa, huku makondakta wakiwafuata askari hao nyuma ya mabasi hayo.

Wengine huwa wanajiuliza, kama kuna kosa kwenye gari, kwa nini asishuke dereva aambiwe, badala yake anashuka kondakta anakwenda kuwafuata nyuma ya basi kwa dakika mbili na kuondoka.

Lakini pia askari hao wamepachikwa majina mengi na madereva na makondakta ambayo wao hawajui, yakiwamo ya 'watu wa njaa',na mengine mengi hali ambayo inaonyesha dharau.

Jambo la muhimu ili kuendelea kuheshimika, ni wao kujisahihisha kwa kuzingatia kwamba, Rais amekuwa akikemea vitendo hivyo, na ikumbukwe kuwa Rais ana vyanzo vingi vya kupata taarifa, hivyo anachoonya kipo.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Asante Mama Samia kwa kusema 'Kusamaheana Kupo', sasa samehe



**Na Pascal Mayalla**

TUNAINGIA katika wiki ya sikukuu ya Krismasi. Kwa baadhi ya watu, sikukuu hii japo ni ya dini ya Kikristo kuadhimisha kuzaliwa kwa Yesu Kristo, zaidi ya miaka 2000 iliyopita, ni siku kubwa kwa mataifa yote.

Krismasi husherehekewa kifamilia zaidi. Kwa nchi za wenzetu wanajiandaa kwa mwaka mzima kuja kusherehekea sikukuu hii. Kwa baadhi ya ofisi hasa za kimataifa, hutoa mshahara wa 13. Kwa mwezi huu, wafanyakazi hulipwa mishahara miwili na hulipwa mapema ili kuwawezesha kusherehekea Krismasi na familia zao.

Kwa baadhi ya makabila, yenye hali nzuri kiuchumi wakiongozwa na Wachagga, Krismasi husherehekewa kwa kwenda Moshi na kujiunga na ndugu zao vijijini.

Wakati wengine tukijiandaa kusherehekea sikukuu hii kwa furaha, kula na kunywa na kufurahi na ndugu, jamaa na marafiki, kuna Watanzania wenzetu, sikukuu hii wanailia magerezani wakiwa wafungwa au mahabusu.

Mmoja wa watu katika kundi hilo ni Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe. Yuko mahabusu kutokana na kesi ya ugaidi inayomkabili.

Wakati ninaandika nakala hii, ninajua sheria inazuia kujadili kesi zilizoko mahakamani ili kutoingilia uhuru wa mahakama. Hii ni kwa mujibu wa Sura ya 16 ibara ya 114.

Hata hivyo makala hii haijadili mwenendo wa kesi yoyote kwa mana ya kuingilia uhuru wa mahakama bali itataja mazingira ya kesi yenyewe ambayo ni ya jinai lakini imegubikwa na siasa.

Mfumo wa mashtaka nchini, uko chini ya mtu anayeitwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ambaye anateuliwa na Rais kwa mujibu wa Ibara ya 59 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Huyu ndiye mtu pekee mwenye mamlaka yote kuanzisha na kuendesha mashtaka yote ya jinai.

DPP pia amepewa mamlaka chini ya kifungu cha 90 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Ana mamlaka ya kuanzisha mashtaka yote ya jinai dhidi ya mtu yeyote mbele ya mahakama zote (isipokuwa mahakama ya kijeshi na mahakama ya katiba). Kifungu cha 91 kimempa DPP mamlaka ya kuondoa mashtaka dhidi ya mtuhumiwa yoyote na kifungu cha 98 kinampa mamlaka kumfutia mashtaka mtuhumiwa yoyote kwa kutumia kitu kinachoitwa 'Nolle Prosequi'. Uamuzi wa DPP hauingiliwi, wala kuhojiwa na mamlaka yoyote, hata Rais.

Kwa mantiki hiyo, DPP ni mtu mwenye mamlaka kubwa sana. Mtu mwingine mwenye mamlaka ya kufanya lolote bila kuwajibika kutoa sababu zozote kwa yeyote ni Rais wa Tanzania. Kwa mamlaka hayo, ni DPP pekee ndiye anayeweza kufanya mtu akale krismasi na familia yake au alie gerezani.

Japo kesi hii ni ya jinai na jinai haina muda maalumu, inadaiwa kutendwa wakati wa utawala wa awamu ya tano.

Uchunguzi ulifanywa kipindi hicho, baadhi ya wahusika wakakamatwa kipindi hicho, wakahojiwa, wakaandika maelezo, wakashikiliwa mahabusu.

Mtuhumiwa mkuu hakukamatwa, hakuhojiwa, hakuandika maelezo lakini alipoanza kuhamasisha katiba mpya, ndipo alipokumbukwa, akakamatwa na kuunganishwa na wenzake.

Wiki iliyopita katika mkutano wa vyama vya siasa, Kiongozi Mkuu wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, aliibua suala hilo mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Rais alitoa jibu la kutia moyo sana na kuleta matumaini mapya kuwa "kusameheana kupo". Zitto anastahili pongezi kwa kuliibua hili.

Pongezi zingine anastahili Mama kwa kauli kwamba kusameheana kupo. Sasa tunakuomba Mama samehe tu hata kama anayestahili kusamehewa ni toto tundu.

Tunaijua karma na utendaji wake, hivyo tunapaswa kumpongeza kwa kufanya vitu vinavyoweza kuleta karma nzuri. Ni vyema tukajua vitu vinavyoweza kuleta krma katika maisha. Kitu cha kwanza kuleta karma mbaya ni kufanya kitendo chochote kitakachoondoa uhai wa mtu, kitu cha pili ni ukosefu wa haki.

Kwa upande mwingine, kitu kinachoongoza kuleta karma nzuri ni kumcha Mwenyezi Mungu na kuzishika amri zake.

Cha pili ni kutenda mema, kutenda haki na kusamehe hata bila kuombwa msamaha. Kutokana na hali hiyo, tunamwomba mama asamehe tu, mtu ale Krismasi na familia yake.

Rais Samia alizungumzia hili kuwa kusamehe kupo. Kwa mujibu wa katiba yetu, sheria zetu, taratibu na kanuni, Rais hawezi kumsamehe mtuhumiwa yeyote wakati kesi iko mahakamani. Huko kutakuwa kuingilia uhuru wa mahakama. Uwezo wa Rais ni kumsamehe mfungwa yeyote baada ya kuhukumiwa.

Mtu pekee mwenye mamlaka ya kuingilia kesi yoyote ya jinai, ikiwa hatua yoyote kabla ya hukumu ni DPP. Maadam Rais Samia ameishaona nia njema kuhusu hili, kilichobaki ni DPP ama aamue kuitekeleza nia njema ya Rais kwa kufanya anachotakiwa kufanya.

Kwa vile kwa mujibu wa katiba DPP hapaswi kuingiliwa, kuelekezwa au kushinikizwa na yeyote, mpira huu sasa umetua mguuni kwake. Amebaki yeye ya goli tu ama apige afunge bao, hili liishe, au apige ndefu mpira upae juu ya goli, mechi iendelee.

Mheshimiwa DPP, nimalizie kwa kukupongeza kwa kazi kubwa nzuri iliyotukuka uliyoianza ya kumwaga 'Nolle' za kutosha.

Watanzania wanamkubali sana Madam Rais juu ya kujitolea kwake kwa dhati ya moyo wake kuliponya taifa kwa kuhakikisha Watanzania wanatendewa haki.

Nakuomba kama itakupendeza, utumie uwezo wako na mamlaka yako ya kutumia Nolle kulimaliza na hili, bila kuonyesha nia tunakupangia au kukushinikiza.

**Nawatakia heri ya Krismasi.**

**Pascal Mayalla**
**pascomayalla@gmail.com**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tusiendekeze, kuchekelea ajali hizi asilani



**Na Joseph Kulangwa**

**Kipanya hiki ni cha kubeba na kusafirisha magazeti kutoka Dar es Salaam kwenda Nyanda za Juu Kusini. Kikaua Watanzania tisa papo hapo na wengine watatu kujeruhiwa na kulazwa hospitalini.**

TUKO mwishoni mwa mwaka, katikati ya mwezi wa mwisho wa mwaka. Huu ni mwezi wenye sikukuu na mbilingembilinge nyingi zikiwamo za maandalizi ya watoto kuanza au kurudi shule.

Ni mwezi wa kila mmoja kujipanga kisawasawa, kwa ada za shule na kodi ya pango kwa wapangaji wa wenye nyumba zao. Lakini pia ni mwezi unaokubuhu kwa ajali za barabarani.

Tayari hadhari zimetolewa na wenye dhamana ya usalama barabarani kuhusu safari zisizo za lazima lakini kama zitahitajika basi uangalifu kwa vyombo vya moto na alama za barabarani uzingatiwe.

Polisi kwa hilo ndiyo hasa dhamana yao nikimaanisha polisi wa usalama barabarani, maarufu kama trafiki. Wana jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa mwaka unamalizika bila damu kumwagika barabarani, kutokana na sababu nje ya uwezo wa binadamu au uzembe wa madereva pamoja na ubovu wa barabara na vyombo vya moto.

Nayasema haya baada ya kuwa tumeshuhudia tayari ajali mbaya ya barabarani mkoani Iringa, ambako roho za watu tisa kati ya 12 zilipotea katika ajali iliyohusisha basi dogo aina ya Toyota Hiace. Wanaita kihaisi au kipanya.

Kipanya hiki ni cha kubeba na kusafirisha magazeti kutoka Dar es Salaam kwenda Nyanda za Juu Kusini. Kikaua Watanzania tisa papo hapo na wengine watatu kujeruhiwa na kulazwa hospitalini.

Polisi wakasema kiini cha ajali hiyo ni mwendokasi wa gari uliosababishwa na dereva, kwani kipanya hicho kilipamia mti pembeni mwa barabara usiku na kusababisha janga hilo lililoshitua wengi.

Ina maana ajali hiyo haikuweza kuzuilika, kwa sababu kwanza ulikuwa usiku, lakini pia hakukuwa na polisi wa usalama barabarani maeneo hayo nyakati hizo, kwa sababu usiku huwa hawamuliki tochi zao.

Pengine ingekuwa mchana ajali hiyo isingetokea, kwa sababu mchana ndio wakati trafiki wamejiwekea utaratibu wa kufanya kazi na usiku kama hawalali basi wanakuwa na kazi nyingine.

Kazi hiyo ni ya kusimamisha magari na kusachi madereva kwa ajili ya kitu kidogo. Hao ni polisi wasio waaminifu ambao hudhani kazi yao ni kutafuta rushwa kwa madereva, na si kuzuia au kupambana na ajali.

Hivi kwa nini magari hayo ya magazeti yabebe abiria tena usiku? Kwa nini yakimbie mwendokasi hivyo na kusababisha maafa? Je, polisi hawajui kuwa kuna magari hayo yanayokiuka usalama wa barabara na kusababisha hayo?

Bila shaka wanajua, lakini wanachokitumia ni kitu kidogo kwa madereva, huku wakijidanganya kuwa usiku ni wakati wa dhambi tu, pokea kilicho chako mwachie dereva akimbie, akipata ajali ni yeye na Mungu wake.

Huo umekuwa sasa ni utaratibu kuwa kuna magari yasiyo rasmi yanasafirisha abiria usiku, tena kutoka maeneo yanayojulikana, kama vile Ubungo, Kimara na Mbezi kwenda mikoani bila tiketi wala kumbukumbu yoyote.

Magari haya ni pamoja na yanayotoka ng'ambo na kupitia nchini kwenda nchi za nje.

Ni magari ama ya mitumba au mapya yanayoshushwa bandari ya Dar es Salaam na kusafirishwa, haya ni maarufu kama 'IT'.

Hayo na ya magazeti yanapita walipo polisi na kuacha kitu kidogo na kuruhusiwa kuendelea na safari zao tena kwa kasi ya ajabu, na yanapopata ajali kila mtu na hamsini zake, ajali zitapimwa watu watapewa taarifa na yatakwisha.

Ina maana gani chombo kama Polisi kilichopewa dhamana ya kulinda usalama barabarani, kiache magari haya yaendelee kubeba abiria badala ya magazeti, au kusafirishwa yaendako badala ya kubeba abiria?

Kitendo cha kuachwa magari haya yapite usiku na kwenda kuua watu, hakikubaliki. Maana yake ni kwamba sasa Jeshi la Polisi likae chini na kujipanga hata kwa kuweka vizuizi barabarani usiku na kukagua kila gari lipitalo na kujiridhisha.

Hiki ni kipindi cha baadhi ya watu kusafiri kwenda kwao eti kuhesabiwa, hivyo kila mmoja anafanya awezalo asafiri na akosapo usafiri halali hupanda haramu kama hivyo, na itokeapo ajali ndipo huanza kukodoleana macho. Ikomeshwe hii kwa usalama wetu. Alamsiki!

SAFU

## KONA YA UKWELI



Na Thobias Mwanakatwe

# Wanasiasa wamwelewe Rais Samia demokrasia ni kuheshimu sheria

DESEMBA 15, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi katika mkutano wa wadau wa kisiasa waliokuwa wakijadili hali ya demokrasia nchini.

Katika mkutano huo Rais Samia alizungumza mambo mengi ambayo kimsingi yamezua mjadala mkubwa nchini kuhusu wanasiasa.

Baadhi ya mambo aliyoyazungumza ni suala la kuheshimu sheria, heshima ya mtu kwamba inakuja kwa kuheshimu sheria za nchi.

Bila kuuma maneno, Rais alisema demokrasia ni kuheshimu sheria, uvunjifu wa sheria unavunja heshima ya serikali inashindwa kukuheshimu. Kusameheana kupo. Alisema kuna umuhimu wa kuzungumza na kufikia maridhiano ya kuzizika tofauti.

Pia alisema tunapaswa kubishana kwa hoja za kizalendo zinazoendana na uhalisia wetu kiutamaduni, kiuchumi na kijamii kwa kuwa jambo la busara ni kuondoa kasoro kwa kuelekezana, kuelimishana na kujadiliana.

Nianze kwa kumpongeza Rais kwa maneno yake mazuri na ya busara kwa wanasiasa. Nina imani kama watayazingatia basi siasa za nchi yetu zitakuwa za kiwango bora kabisa.

Baada ya hotuba hiyo,kumeibuka mijadala mingi kwenye mitandao ya kijamiii ambapo kimsingi ukiifuatilia ni kama vile wanasiasa hawajamwelewa Rais Samia. Rais amesema anataka muafaka, kaongelea kusamehe, amekiri mikutano ni haki ya wanasiasa. Sambamba na hiyo. amekubali kuwe na 'dialogue'.

Wanasiasa lazima watambue kuwa wananchi wanaunga mkono demokrasia si kwa sababu ni kitu muhimu kwa chenyewe, bali pia wanatarajia demokrasia iwapatie maisha bora ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Hili lilionekana wazi hata wakati wa maandamano ya mapinduzi nchi za Uarabuni mwaka 2011, pale watu wengi walipomwagika mitaani na kwenye viwanja mbalimbali ili kushinikiza serikali zao kuwapatia mahitaji yao muhimu na haki za binadamu huku wakiimba, kwa mfano, kwa kaulimbiu kama vile "mkate, uhuru na utu".

Watu wanatarajia serikali zao kutoa huduma za umma kwa ufanisi mkubwa na ambao utakidhi mahitaji yao na kutambua haki zao kama binadamu lakini inapotokea wanasiasa wanakuwa kikwazo kwa serikali wanakuwa hawawatendei haki wananchi.

Serikali zinazowajibika kwa wapiga kura, au wawakilishi na vyombo vya usimamizi, kama vile bunge, vyama vya kisiasa au taasisi kuu za ukaguzi wa hesabu zenye uwezo wa kuzishawishi taasisi hizo, ina uwezo wa kutimiza matakwa ya wananchi kuliko serikali ambazo haziwajibiki.

Wanasiasa wafahamu kuwa nchi zenye viwango vya chini vya utoaji wa huduma zinafanana katika jambo moja hazina sheria au zina sheria dhaifu katika kuwapa adhabu au kuwapa tuzo wale wanaofanya vizuri.

Ikumbukwe nchi nyingi za kiafrika ambazo zimeingia katika vita chanzo chake kimetokana na wanasiasa ambao hawataki kuzingatia sheria na katiba ya nchi.

Wanasiasa wafahamu kuwa mfumo wa vyama vingi ulipoanzishwa mwaka 1992 lengo lake ilikuwa kuleta demokrasia ya ushindani wa kisiasa ili kuleta maendeleo katika nchi husika.

Uwapo wa mfumo huu katika baadhi ya nchi unasaidia na hata hapa kwetu umesaidia kukiangaliza chama kilichopo madarakani.

Kwa msingi huo, vyama vya siasa vipo kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. Walioko katika vyama vingi,wanatekeleza haki yao na wajibu wao wa kikatiba, na kama raia.

Kama vile ambavyo wana haki kwa mujibu wa Katiba na sheria za vyama vingi vya siasa, pia wanao wajibu. Lakini swali la kujiuliza je misingi ya kuanzishwa kwa vyama vingi vya siasa inazingatiwa na vyama husika.

Tangu kuanzishwa kwa vyama vingi, nimekuwa nikishudia kukiukwa kwa misingi ya kuanzishwa kwa vyama vya upinzani kutokana na baadhi ya viongozi wa vyama hivyo kutumia vibaya uhuru wao na kuhatarisha usalama wa nchi.

Wako baadhi ya wanasiasa na vyama vyao badala ya kusimama katika misingi ya kidemokrasia lakini wao wamekuwa ndo wachochezi wakubwa wa vurugu hapa nchini na wengine kuichafua nchi kimataifa kutokana na maslahi yao binafsi ya kisiasa.

Chama cha siasa si kwamba ni lazima upinge kila kitu na hapo ndipo tunashuhudia kuwa vyama vya siasa vingi vimepotoka na kuondoka kabisa kwenye mstari wa misingi ya kuanzishwa kwa vyama vya siasa.

Wakati umefika kwa vyama vya siasa viongozi wake wahakikishe wanakuwa wazalendo kwa nchi yao kwa kufanya siasa za kistaarabu ambazo hazitasababisha nchi yetu kuingia katika machafuko yasiyo ya lazima.

Wanasiasa mrejee hotuba ya Rais Samia muisome na kuisikiliza kwa makini hata mara 10 mtamwelewa alichokuwa akimaanisha badala ya kujifanya hamjamwelewa na kuendelea kupayuka.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

# KUINGILIA NDOA ZA WATOTO NI SUMU -2

KATIKA sehemu ya kwanza ya makala hii nilibainisha kwamba wazazi wengi wamesahau kuwa ndoa ni taasisi huru inayojitegemea. Hii ni kutokana na baadhi ya wazazi na ndugu kuchangia kuvurugika na kuvunjika kwa ndoa za watoto wao badala ya kusaidia kuzidumisha.

Pia nilieleza kuwa katika ndoa kuna kanuni tatu ambazo wanandoa, wazazi na ndugu wanapaswa kuzingatia. Kanuni hizo ni Kuacha, Kuambatana na kuwa wamoja.

Kuhusu kanuni ya kuacha, ina maana zaidi ya kuondoka na kwenda kuishi mahali pengine na mke au mume. Hii inamaanisha kuwa tangu siku ya harusi, uhusiano wa mwanamume na wazazi au ndugu zake unapunguzwa na uhusiano mkubwa utakuwa na mke au mume wake. Neno kuacha linabadili uhusiano wa kibinadamu uliozoeleka kabla ya ndoa.

Mwanamume anapooa, uhusiano wake na mkewe ni jambo la msingi na kipaumbele cha kwanza. Kwa msingi huo, vijana wanapoandaliwa kuingia katika maisha ya ndoa wanahitaji kuandaliwa kisaikolojia kukabili badiliko hili. Kwa mantiki hiyo, vijana waandaliwe kuondoka, kujitegemea na kuwa na uhuru wa kuendesha maisha yao ya ndoa bila kuingiliwa. Aidha, Wazazi wao nao wanahitaji kufahamu badiliko hili muhimu.

Wanandoa wanapaswa kuwa na uhuru na faragha binafsi, uhuru katika kufikiri mambo yenye faida kwao wawili na ndoa yao, uhuru katika kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu maisha yao na wazazi wao au ndugu zao, uhuru katika mapato yao na matumizi yao kwa ustawi wa familia yao.

Pia Wanandoa wanakuwa na mamlaka na utawala kamili. Kwa hiyo, Wanandoa kuendelea kuwa tegemezi kwa wazazi wao, kuishi kwa mashinikizo na kuongozwa na watu wengine ni dalili ya kutokukua. Hali hii huondoa uhuru na kujiamini kwa wanandoa katika kuendesha na kusimamia maisha yao ya ndoa.

Mtu akiwa ameoa au kuolewa maana yake ni kwamba, amekuwa mtu mzima mwenye maamuzi. Hivyo, mwanandoa kusubiri kuambiwa afanye nini au kufuata kila kitu wazazi au ndugu wanachotaka au wasichotaka, ni kuikosea ndoa na matokeo yake ni misuguano na ugomvi ndani ya ndoa, kwani nafasi ya mwenzi inakuwa haipo tena.

Baba au Mama, kaka au dada wanastahili kuheshimiwa nasi kama binadamu kwanza, halafu kama ndugu au wazazi. Lakini, kuwa ndugu au wazazi hakuwapi watu hawa haki na mamlaka ya kuingilia ndoa ya watoto wao au ndugu zao.

Pamoja kwamba mtoto hakui kwa mzazi, lakini inapofikia hatua ya ndoa, kuna mipaka ya kutunzwa na kuheshimiwa na wazazi ili ndoa ikue. Kukua ni pamoja na kujua kwamba, hata mzazi anaweza kukosea kama binadamu mwingine yoyote.

Ni vema ifahamike kuwa, Kuacha haimaanishi kutelekeza au kuondoa nafasi ya wazazi kwa watoto wao, bali kutoa uhuru kwa watoto wao waliooana kuendesha maisha yao ya ndoa bila kuingiliwa wala kupokea amri kutoka kwa wazazi.

Kufanya hivyo ni sehemu ya kuheshimu mipaka na ndoa ya watoto wao na kutambua kuwa, sasa ni watu wazima wenye uwezo wa kufanya maamuzi na wenye majukumu mapya.

Wazazi wanaweza kutoa ushauri pale unapohitajika na sio kutoa amri. Kama ushauri unakusudia kujenga na kuimarisha maisha ya ndoa ya watoto wao badala ya kuwavuruga, unaweza kupokelewa.

Wanandoa kama watu wazima, wanao wajibu wa kupima kila ushauri unaotolewa au maneno wanayoelezwa na mtu yeyote yule, kwani wakati mwingine ndoa huvurugwa na ndugu, wazazi, marafiki, majirani, wafanyakazi wenzetu, yamkini hata wale tunaoabudu pamoja nao. Kumbuka, mara nyingi watu wanaoweza kukuumiza huwa hawatoki mbali, mara nyingi huwa ni wale walio karibu nawe.

**KUAMBATANA**

Baada ya kuangalia kanuni hiyo, sasa tukijite na ya pili ambayo ni kuambatana. Katika ndoa kuna kuambatana (cleave). Maana yake ni kushikamana au kung'ang'aniana. Kuambatana na mke inamaanisha kuwa, mwanamume ana utambulisho mpya ambao ni uhusiano na mkewe na sio wazazi wake.

Hii maana yake ni mume awe na uhusiano mkubwa na wa karibu zaidi na mkewe kuliko watu wote wengine. Vivyo hivyo, mke inampasa kuhusiana na mume wake zaidi kuliko watu wote wengine. Mtu wa kwanza wa kuhusiana naye, wa kumpenda na kumthamini (baada ya Mungu) awe ni mkewe, na mke vivyo hivyo kwa mumewe. Baada ya Mungu, mke au mume apate nafasi ya kwanza kabisa na ya maana katika moyo wa mwenzi wake.

**KUWA WAMOJA**

Katika ndoa wanandoa wanapaswa kuwa wamoja na kuishi kwa umoja. Hii inamaanisha kuwa mume na mke wana uhusiano wa pekee kati yao. Ni watu wanaotegemeana.

Mume na mke wameungana kiroho, kiakili, kimwili, kihisia, kimapato, na mambo mengine. Mke anatimiliza kilichopungua kwa mumewe, kama jinsi sifa za mke zinavyokamilisha zile za mume.

Katika ndoa ambayo mume na mke wameunganika kwa namna hii, ni sawa kwamba mtu mpya kamili ameumbwa. Kila mmoja anakuwa sehemu ya mwenzake na wanafanya kila kitu pamoja kwa umoja. Washirikiana na kila kitu walichonacho kinakuwa ni kwa ajili ya wote.

Kabla ya ndoa kila mmoja alikuwa akifikiri na kutenda binafsi. Lakini baada ya kuoana, mambo yote, ikiwa ni pamoja na yale yanayohusu kutoa misaada kwa wazazi, ndugu na watu wengine, yanapaswa kufanywa kwa kushirikiana, kushauriana na kukubaliana. Katika ndoa hao wawili wameunganika, na neno "mimi" linachukua maana nyingine na kumaanisha "pamoja na mwenzi wangu". Umoja ni kinga dhidi ya saratani ya ubinafsi katika ndoa.

Furaha katika ndoa hutengenezwa. Dhana ya kuacha, kuambatana na kuwa wamoja vinapozingatiwa katika ndoa huleta furaha na kuepusha migogoro isiyo ya lazima katika ndoa. Mafanikio katika ndoa yanahitaji jitihada ya mume na mke. Ni muhimu mume na mke kwa pamoja watamani na kudhamiria ndoa yao kukua na kuwa yenye furaha.

**■Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

DESEMBA 19, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


**X-mas na nyama choma**



Ukurasa 15

## NYUMBA:

Namna ya kupamba nyumba yako msimu huu wa sikukuu




## KATUNI

Ukurasa 16




NGOZI KAVU

# Tatizo la wengi lakini linaisha

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | J | U | M | B | A |
| | A | | | O | |
| U | M | O | | M | |
| | B | | P | A | A |
| | I | | | N | |
| K | A | M | B | I | |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
BEI, UMA, WANGA, DUNDA, DUMAZA, DEREVA

## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya Adaktari

MTOTO Juma alikuwa na baba yake wakila chakula cha usiku, wakati wanaendelea kula alianza kumuuliza baba yake maswali mbalimbali.

Baba Juma aliendelea kujibu maswali ya kitoto kutoka kwa mwanawe huku wakitabasamu na kuonekana kama mchezo wa kufurahisha.

Juma: Baba yani ninapokula chakula unachonunua wewe nitapata matatizo?

Baba: Hapana mwanangu nina wajibu wa kukutunza wewe na mama yako

Juma: Lakini mwalimu alituambia darasani kwamba mtegemea cha ndugu hufa masikini.

Baba: hahaha...Hapana mwanangu huo ni msemo tu unamaanisha kila mtu kufanya kazi kwa bidii ili kupata maendeleo.

SWALI

Wadudu aina ya senene ni chakula chenye lishe kinapatikana mkoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Kulikoni mke wa pili atese watoto aliowakuta na baba yao?

KARIBU tena msomaji wangu tujumuike kwenye safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo hebu tumulike yanayojiri kwenye familia zetu. Tujiulize, hivi ni kwa nini mwanamke aliyeolewa mara ya pili hunyanyasa watoto aliowakuta?

Hili ni swali linalowatesa wanaume walio wengi. Kila wakitafakari hawapati jibu lililonyooka. Hata hivyo, kina baba hawa wanashindwa kuelewa kwamba hakuna jambo linalotokea kwa bahati mbaya.

Msomaji wangu, hebu sikia toka kwa mmoja wa wasomaji wetu kupitia ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani, akisikitishwa na tabia ya baadhi ya wanawake kutesa watoto wa wanawake wenzao.

Anasema hivi: "Asante kwa ujumbe maridhawa kwenye makala yako. Swali langu ni kwa nini wanawake wengi hupenda watoto walioenda nao kwenye ndoa ya pili, watunzwe vizuri na kunyanyasa watoto waliowakuta kwenye ndoa ya pili? Joseph wa Chato, Geita."

Msomaji wangu, kila nikitafakari ujumbe huo hapo juu, naona chanzo kikuu ni roho ya mitaala. Roho hii husababisha ndoa za wake wengi, kuolewa na wanaume wengi, kuoa na kuacha au kuachika. Roho hii husababisha kukosekana kwa upendo kati ya wanandoa, ugomvi usioisha kati ya wanandoa na kuwafanya watu wengi wajane katika umri mdogo.

Tukirudi kwenye swali ya msomaji wetu, kwa nini baadhi ya wanawake hutesa watoto waliowakuta katika mji ambao wao ni ndoa ya pili. Yaani alikuwepo mama akaondoka, kisha yeye akaingia kama mke wa pili.

Nimetangulia kuielezea roho ya mitaala jinsi inavyofanya kazi na maafa inayosababisha. Ukiona mwanamke ameolewa kisha akaondoka, huyo anafuatiliwa na roho ya mitaala. Na yule mwanamke anayeingia kwenye nyumba ambayo tayari alishakuwepo mwanamke akaondoka, kadhalika naye roho ya mitala inamhusu.

Kwa mantiki hiyo, wanawake wa aina hii hawaondoki au kuingia kwenye nyumba hizi wakiwa watulivu, huwa wamevurugwa. Lazima aliyeondoka alitoka kwa ghadhabu na huyo aliyeingia anayo mapungufu yake. Na mbaya zaidi ni yule anayeingia ndoa ya pili akiwa na mtoto au watoto.

Wanaume ni watu ambao hawana mambo mengi. Anapopenda anamaanisha upendo wa dhati. Anaamini kuwa mke yule pia anao upendo toka rohoni. Lakini kumbe mke huyo akawa na roho mbaya zilizojificha kama hiyo ya mitala, umasikini,uongo, mizimu, uzinzi, uvivu na ujinga.

Endapo mwanamke amebeba kati ya roho hizo hapo juu, atajikuta anakimbia ndoa yake bila kujielewa. Wapo wanawake wamehama na watoto na wengine huwaacha na baba yao. Na kwa sababu baba huyu ni mtafutaji, inamlazimu atafute mtu wa kuwaangalia watoto wakati hayupo.Na pale anapobahatika kupata mke mwingine, ndipo huanza kuwanyanyasa watoto aliowakuta badala ya kuwalea kama watoto wake. Mbaya zaidi kama naye ana watoto upendeleo ni mkubwa kwa wale aliowazaa kuliko aliowakuta.

Msomaji wangu, wanawake ni watu wanaopaswa kuwa na upendo katika familia zetu. Mwanamke ni mzazi na mlezi na pia kiongozi msaidizi katika kaya zetu. Watoto wanatarajia malezi mazuri na hasa mama ambaye muda mwingi yupo karibu nao.

Sasa watoto wanapoona mama anaonea au kunyanyasa, anabagua watoto na kuonyesha upendeleo wa wazi katika mavazi na mahitaji mengine kama chakula, ni jambo linalowaacha na maswali mengi na mshangao hata kwa jamii inayowazunguka.

Watoto ni viumbe waoga. Pia huamini kile mzazi anachofanya au kutamka ni sahihi wanapokuwa katika umri mdogo, ule ambao hawajaweza kutofautisha jema na baya. Ndio maana katika malezi lazima mzazi au mlezi awe makini ili asimlishe mtoto maneno mabaya.

Utasikia mtoto anatamka tusi baya, ukimuuliza umesikia wapi anataja mama au baba na pengine dada. Mtoto huyu aliamini kuwa ni maneno mazuri kumbe ni matusi. Na mtoto ukimfanyia ukatili hawezi kuusahau.

Jambo moja ambalo wengi wetu hatuelewi ni kwamba kile unachokitengeneza leo, utakutana nacho baadaye. Maisha Ndivyo Yalivyo! Siku zote Mungu hapendi uonevu, ni mwenye haki. Kwenye malezi upendeleo ni sumu!

Watoto wote walelewe kwa usawa. Hao ni ndugu watakutana huko baadaye na kusaidiana. Niishie hapa. Je, una maoni, Kisa! Tuma ujumbe mfupi 0715268581.

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Tuchukue tahadhari wakati kirusi kipya kikisambaa duniani

DUNIA inataabika na kirusi kipya cha corona kiitwacho omicron kilichogundulika Novemba 24, mwaka huu, nchini Afrika Kusini na baadaye kuonekana Ubeligiji, Hong Kong, Israel na Botswana.

Pia kinaendelea kusambaa kwa kasi kubwa na sasa Shirika la Afya Duniani (WHO) linasema hakiwezi kudhibitiwa bali kila mtu ahakikishe anafuata taratibu za afya kwa kuvaa barakoa, kuepuka misongamano na kusafisha mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni.

Hali hii inakuja ikiwa dunia haijapata tiba ya kirusi cha awamu ya kwanza hadi ya tatu ambavyo vimeumiza wengi na mamilioni kupoteza maisha, kufilisika na mifumo ya afya ya nchi mbalimbali kuelemewa.

WHO ilisema kirusi cha kwanza kilionekana kuonyesha dalili nyingi ambazo ni rahisi kutambua na kudhibiti ambazo ni koo kuwasha, homa, mwili kuchoka na maumivu ya kifua ambayo huonekana ndani ya siku 14.

Kirusi kipya wakati mwingine mtu anaumwa na hawi na dalili yoyote bali hujisikia mchovu au mwili kuuma jambo ambalo ni gumu kujitambua.

Aidha, kirusi hiki kinaibuka wakati dunia inaendelea kupona majeraha ya corona awamu ya kwanza ambayo imeathiri uchumi wa dunia,nchi na mtu mmoja mmoja,kwa kuwa kuna sekta nyingi kama za utalii zimeathirika kutokana na kwamba idadi ya wageni imepungua maana yake na mapato nayo yameporomoka.

Hadi sasa China haijafungua mipaka yake hali inayoathiri wafanyabiashara na wananchi wa kawaida kwa kuwa mizigo haiji tena kwa wingi na ubora unaotakiwa. Bei zinapanda na wengine kupata hasara kutokana na kutapeliwa au mizigo kuchukua muda mrefu kwenye usafiri wa majini.

Nchi zimelazimika kubadili bajeti huku waajiriwa wakipunguziwa mishahara au wengine kuondolewa kazini kabisa kwa kampuni au mashirika kupunguza matumizi au kufunga kutokana na kushindwa kuendelea na kazi.

> **Ni muhimu jitihada za udhibiti mipakani zikaongezeka,kama utaratibu wa nchi ulivyo kwamba kila anayeingia na kutoka ni lazima apimwe corona, pamoja na kuhamasisha uvaaji wa barakoa na kutumia vitakasa mikono mara kwa mara.**

Sasa kirusi kipya kiko duniani, Tanzania si kisiwa ni lazima kuchukua tahadhari zote muhimu ili kuepusha madhara makubwa yanayoweza kuwapata wengi.

Ni muhimu jitihada za udhibiti mipakani zikaongezeka,kama utaratibu wa nchi ulivyo kwamba kila anayeingia na kutoka ni lazima apimwe corona, pamoja na kuhamasisha uvaaji wa barakoa na kutumia vitakasa mikono mara kwa mara.

Pamoja na yote lazima kuendelea na jitihada za kumuomba Mungu aiponye nchi na dunia kwa kuwa zipo shuhuda kwenye vitabu vitakatifu Mungu aliiponya dunia dhidi ya ugonjwa wa tauni uliowatesa wengi miaka hiyo, hivyo kama alifanya kwa wale hata sasa atafanya kwa dunia ya leo.

Kila mmoja kwa imani yake akimlilia Mungu atauweka mkono wake mkuu na kuiponya dunia,tunaeleza Mungu alipotaka kuliponya taifa alitafuta maelfu hakupata,mamia na baadaye alimpata mmoja aliyesimama kwenye imani ya kweli,nasi leo tunafundishwa kusimama katika imani na Mungu atasikia sala zetu ataliponya taifa na dunia.

Mwenyekiti wa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala Tanzania, Prof. Hamis Malabo, alikaririwa kuwa asilimia 60 ya dawa za kisasa zinatokana na dawa za asili ambazo ni mimea lakini zinapuuzwa.

Alisema tiba asili ni muhimu na hata taarifa zilizowekwa awali kwenye tovuti ya WHO zilionyesha dawa hizo zinaweza kutumika kukabili maradhi hayo,ingawa baadaye ziliondolewa.

Hivyo basi,ni wajibu wetu kila mmoja kumuomba Mungu,kuchukua tahadhari na kuendelea kufanyakazi kwa bidii ili kuzalisha mali huku tukiendelea na maisha kwa kuwa corona ipo na tutaendelea kuishi nayo.

Kwa sasa ubunifu unafanyakazi na ndiyo maana sasa vikao vingi vinafanyika mtandaoni,lakini tunaona kasi ya ukuaji wa teknolojia kwa manufaa ya watu wote.

Tuchukue tahadhari kwa kufuata ushauri wa wataalamu wa afya ili tuendelee kuwa salama vinginevyo tutaingia kwenye mzigo wa matibabu,kupoteza nguvu kazi na kuyumbisha uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

**Mungu Ibariki Tanzania**

**0000**









Ilikuwa siku ya kukumbukwa kwa Ibrahim Felix Temba baada ya kuamua kufunga ndoa na Mary Joseph Matemba katika kanisa la Kristu Mfalme Tabata jijini Dar Es Salaam hivi karibuni, kisha kufuatia sherehe kabambe ya kuwapongeza iliyofanyika Green Hotel.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



# KAUNDA SUTI ILIVYOTETEMESHA 2021

VAZI la aina ya 'kaunda suti' limekuwa maarufu kwa kipindi kirefu, lakini kwa mwaka 2021 limekuwa miongoni mwa vazi lililopendwa na wanaume kutokana na kuwepo na mabadiliko makubwa kiubunifu.

Wabunifu wamefanya kazi kubwa katika kubadilisha muonekano wake wa awali na kuwa wa kisasa zaidi kiasi ambacho lilivaliwa na watu wa rika zote.

Awali kaunda suti ambayo imetengenezwa kiafrika zaidi, alipenda sana kuvaa rais wa zamani wa Zambia Keneth Kaunda, ilivaliwa na watu wa rika ya kati na zaidi kutokana na muundo wake kuwa wa kiheshima zaidi.

Hata hivyo, wabunifu wa mavazi walifanyia marekebisho kadhaa katika kuwafanya watu kuvutika mpaka hadi kuwa katika muonekano wa sasa ambao una mvuto zaidi.

Katika kipindi cha mwaka 2021, kaunda suti imetawala vyema na kufanya kuwa moja ya mavazi yaliyovaliwa na watu wengi zaidi.

Mmoja wa wabunifu, amesema unaweza kusema ulikuwa mwaka wa 'Kaunda Suti' kutokana na kuwa na oda nyingi za watu wanaohitaji na hivyo kujiingizia pesa nyingi.

## UREMBO
Na Mary Geofrey



## NGOZI KAVU
# Tatizo la wengi lakini linaisha

WANAWAKE wengi wenye tatizo la ngozi kavu wanatakiwa kuwa na uangalizi wa hali ya juu, kwa sababu huwa wanakabiliwa na matatizo mengi.

Baadhi ya matatizo yanayoonekana ni mikunjo kutokea hasa kipindi cha baridi na ukavu uliopita kiasi.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, kuna baadhi ya njia unatakiwa kuzifuata ili kupunguza ukavu na kuweka ulinzi wa ngozi.

Namna ya kutunza ngozi

Osha uso wako kila siku na sabuni ya kusafishia uso ambayo haina chemicals na kamwe usitumie sabuni ambayo itaondoa uhasilia wa mafuta kwenye ngozi yako.

Kila siku tumia vilainishaji ngozi wakati wa mchana na unapopaka kilainishi kwenye ngozi yako massage ngozi yako kwa mduara kwa kwenda juu na sio kuvuta au kusugua ngozi yako.

Unatakiwa kupaka mafuta laini (cream) kwenye ngozi yako kabla ya kwenda kulala. Mafuta kama Alpha Hydroxy Acids au AHA`s inajulikana kuwa na wingi wa maziwa, matunda na sukari.

Hizi Alpha Hydroxy Acids, zinakausha, zinaua na zinaondoa tabaka la ngozi ya nje na zinalainisha ngozi mpya inayotoka.

Faida yake ni kwamba ngozi yako inaonekana kuwa nzuri na pia ngozi yako kung`aa na kuwa na rangi nzuri.

Kwa pamoja AHA na Vitamin C husaidi kupunguza nishati na hivyo unaweza kupata matokeo mazuri na kwa haraka.

Kama ngozi yako ni kavu na inaelekea kuwa na mistari, nyekundu na inauma au ina vipele unatakiwa kumuona daktari wa ngozi.

Hali hii pia inaweza kusababishwa na hali ya hewa au kusababishwa na vitambaa kama vile pamba, vitu tunavyopaka kwa ajili ya kutunza ngozi au sabuni na kadhalika.

## MAPISHI
Na Mary Geofrey

# X-mas na nyama choma

NYAMA choma ni nzuri ukiwa unakula kwa ugali na kusukumia kwa vinywaji laini au vikali.

Hata hivyo, unaweza pia kula kama chakula kikuu au kutumia kama kichangamsha kinywa unapokuwa unazungumza na familia au marafiki.

Kuna wanaopenda kula nyama kwa kachumbari ya nyanya, tango na kusindikizwa na chachandu na pilipili kali.

Mahitaji

Nyama ya ngombe kilogram moja au kuku mzima, tangawizi moja, kitunguu swaumu moja, karoti mbili, ndimu moja, pilipili manga ya kusaga na chumvi.

Namna ya kuandaa

Menya tangawizi, vitunguu maji, vitunguu swaumu na karoti.

Weka kila kitu kwenye blender, saga kwa pamoja ili kupata uji mzito.

Weka pilipili manga kwenye mchanganyiko wako.

Chukua nyama yako aina ya kuku, ng'ombe au nyingine unayopenda, kisha weka chumvi.

Kamulia ndimu au limao la kutosha kwenye nyama na kisha changanya kiasi.

Weka nyama kwenye mchanganyiko wako uliotoka kwenye blender.

Weka nyama kwenye jokofu kwa muda wa saa moja au mawili. Unaweza pika kuandaa usiku na kuiacha kwenye jokofu ilale hadi asubuhi.

Andaa mkaa wako kwenye jiko la kuchomea.

Moto ukikolea vizuri, weka nyavu ya kuchomea na tandaza nyama yako kwenye nyavu.

Igeuze mara kwa mara ili iive vizuri pande zote.

Ikishaiva vizuri, weka kwenye karatasi ngumu 'foil paper' ili kuzuia kukauka.

Ukishamaliza kuchoma unaweza kula. Usisahau pilipili, ndimu au limao wakati wa kula.



Na Elizabeth Zaya



# Namna ya kupamba nyumba yako msimu huu wa sikukuu

MSIMU wa sikukuu umewadia, huku kukiwa na pilikapilika za hapa na pale. Katika nyumba kunaonekana kutawala mapambo yanayoshabihiana na msimu wenyewe.

Katika ofisi na sehemu mbalimbali ukipita au kuingia unakutana na mapambo ya sikukuu ikiwamo mti wa Krismasi ukiwa ndio umetawala.

Katika makala hii ya nyumba tunakupa dondoo kidogo kukuongezea baadhi ya vitu ambavyo vitasaidia kuifanya sikukuu yako kuwa nzuri, ukaifurahia ukiwa nyumbani kwako.

Naamini kwamba katika kipindi hiki familia nyingi huwa zinaungana katika mapumziko ya mwisho wa mwaka. Kwa hiyo ni muhimu kukifanya kipindi hiki kikawa ni cha furaha zaidi kwa mapambo tofauti ya siku nyingine ndani ya nyumba.

Mbali na mti wa Krismasi, pia yako mapambo mengine tofauti. kama hutapata mti, unaweza pia kutafuta aina nyingine ya mapambo ambayo huenda yasikugharimu kabisa au ukayapata kwa gharama kidogo.

Lengo ni kuhakikisha nyumba yako inachangamka na kuipa raha familia ambayo imekusanyika nyumbani kwa ajili ya mapumziko.

Unaweza kuchanganya na mapambo mengine tofauti kama 'wooll papers' na mengine kwa kuzingatia rangi zinazoshabihiana na sikukuu pamoja na maua ya kawaida.

Mapambo mengine ambayo yanaweza kutumika Krismasi ni pamoja na karatasi za rangi, taa za kung'aa, mapambo ya karatasi yanayotengenezwa kwa mtindo wa nyota.

Mengine ni kengele za Krismasi, picha za kondoo, farasi, mipira ya kung`aa, wanyama wadogo wa kutengenezwa kama kondoo.

Mapambo mengine ambayo unaweza kutengeneza ni ya maua ya asili kwa kuyaweka katika chupa au chombo maalumu ambacho kinaweza kuwekwa hata juu ya meza.

Pamoja na kupendezesha nyumba, pia hewa na harufu hubadilika na kuwa nzuri zaidi kutokana na maua yanayowekwa ndani.

Unaweza kupamba pia maneno yenye ujumbe maalumu ambayo unaweza kuyaandika mwenyewe ya kuendana na msimu au ukayanunua katika sehemu maalumu yanapopatikana.

Hakikisha unaweka mapambo sehemu ambayo ni salama na hayawezi kuharibika kwa namna yoyote au kuharibiwa na watoto.

Pia nyumba katika msimu huu inatakiwa iwe inapigwa nyimbo zinazoshabihiana na msimu wenyewe.

Baada ya kuisha kwa musimu unatakiwa uyaondoe na kudizaini upya muonekano wa nyumba yako.



## Jinsi ya kupangilia vitu katika kabati



KABATI la nguo kwenye chumba cha kulala ni fenicha muhimu.

Ingawa linajulikana kama sehemu ya kuhifadhi nguo, linahifadhia pia vitu vingine kama viatu, masanduku, mabegi, vitupio vya urembo na mapambo mengine.

Kutokana na umuhimu wake hizi ni baadhi ya dondoo za kupangilia vitu katika kabati la chumbani.


1: Ndani ya kabati kuna vyumba mbalimbali kama vile mashelfu ya juu na chini, madroo, fimbo ya kutundikia nguo na kulabu za kuning'iniza vitu. Hakikisha kila sehemu unahifadhi vitu sahihi ili kuhakikisha kila kitu kinakaa vyema.

2: Jitahidi kutumia henga zinazofanana kwenye nguo zote ulizotundika. Lengo kuu ni matumizi sahihi ya nafasi na kufanya mpangilio uvutie.

3: Panga nguo ndani ya kabati kwa makundi, anza blauzi, jaketi, sweta, makoti,shati, suruali, suti, sketi, gauni, kaptula, fulana na kadhalika.

4: Tumia droo ndogo kuhifadhia soksi na nguo za ndani.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
NIMEKUTOA KITUONI KUJA KUNIKAMATIA MTUHUMIWA WANGU BADALA YAKE UNAMUONA 'UMEGANDA!
WEWE UMENILETA KWENYE MAJARIBU TU!
HUENDI KWENU KUHESABIWA KAMA WENZAKO?
KULE KUNA KUONESHA PESA SIO TUMBO!
"UNASEMAJE WEYE?
BEKA KANUNUA GARI JIPYA AMENIOMBA NIMPE KAMPANI CHRISMASI... NAKUAGA MUME
WAKATI UNABADILIKA MSIISHI KWA KUKARIRI BADILIKENI
TUNATAKA MITI YA KRISIMASI KAMA ZAMANI IUZWE
KWANI ILIKATAZWA?
TUSHANUNUA MITI YA PLASTIKI KILA MWAKA TUNAITOA VUMBI TU
MWAMBIE HUYO! AU ALIKUWA NA TENDA YA KUZOA MITI ILIYOBAKI?
ANATUCHAGIZA HANA LOLOTE!
HATUTAJI VITUO ABIRIA NYIE PIGENI ZOGO
WAPIGIE SIMU WA MJINI WAAMBIE KABISA
WAMENIJIBU KAMA SIKUKUU WAJE NA BAJETI WAMESEMA BASI
HII SASA ZALILI MKE WANGU
UNAJISHAUA SANA KUJIFANYA SIKUKUU UNATEKWA NA KUFICHWA NA MICHEPUKO!
NIMESIKIA KUNA GARI NYEUSI IMEINGIA KWENYE NYUMBA NILIYOPANGI-SHIA 'SMALL HOUSE'
JAMANI KIPINDI HIKI NIPO BIZE NA FAMILIA YANGU MNITAFUTE BAADA YA MSIMU WA SIKUKUU KUMALIZIKA...SAWA NYIE VIJUMBA VIDOGO!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKIWAPISHA UTACHELEWA KUFIKA

HABARI KIMATAIFA

# Ulaya yahaha kuzuia Omicron

**PARIS,** UFARANSA

AINA mpya ya kirusi cha Omicron kinazidi kuleta hofu katika mataifa ya Ulaya baada ya usambaaji wake kuelezwa ni wa kasi kama radi.

Waziri Mkuu wa Ufaransa, Jean Castex, alisema nchi za ulaya huenda ikawa na wagonjwa wengi na hasa Ufaransa kufikia mwanzoni mwa mwaka ujao.

Akizungumza jana saa chache chache kabla ya nchi yake kuweka masharti ya kusafiri kwa watu wanaoingia kutoka Uingereza.

Kufikia jana Uingereza ndiyo nchi iliyoathiriwa zaidi miongoni mwa mataifa ya Ulaya, ikiwa na watu 15, 000 waliothibitishwa kupata maambukizi ya kirusi kipya cha Omicron.

Katika maeneo yote ya bara hilo, maofisa wa afya wanakabiliana na wimbi jipya la maambukizi.

Masharti zaidi ya kuzuia kusambaa kwa virusi hivyo yalitangazwa na Ujerumani, Jamhuri ya Ireland na Uholanzi huku serikali hizo zikitaka kumaliza maambukizi haraka.

Ulaya tayari imeshuhudia visa zaidi ya milioni 89 na vifo vya watu milioni 1.5 vinavyohusiana na Covid, kulingana na takwimu za hivi karibu za EU.

Waziri wa afya wa Ujerumani Karl Lauterbach, aliwaambia waandishi wa habari kuwa taifa hilo lazima lijiandae kwa changamoto ambazo hazijawahi kuwa nayo.

Hata hivyo, shirika lake la afya ya umma likizitaja Ufaransa, Norway, na Denmark kama maeneo hatari kutokana na kuogezeka kwa maambukizi katika nchi hizo.

Ujerumani yenyewe iliripoti zaidi ya visa 42,000 vya maambukizi, vikiwa ni chini ya visa vipya 50,000 vya maambukizi vilivyorekodiwa Ijumaa.

Ireland, ambako theluthi ya visa vipya vimetokana na omicron, Taoiseach Micheál Martin alisema wanatarajia kushuhudia maambukizi ya kiwango ambacho ni zaidi ya kile ambacho kimewahi kushuhudiwa awali.

Tahadhari hiyo inakuja huku Uingereza ikiripoti idadi ya maambukizi kwa siku ya tatu hadi watu 93,000, wengi wao wakiwa na maambukizi ya kirusi kipya cha Omicron.

Ufaransa ilifunga mipaka yake kwa watu wanaosafiri kutoka Uingereza kwa shuguli za biashara na utalii saa tano usiku kuanzia Ijumaa. Kutokana na zuio hilo misururu mirefu ya watu ilishuhudiwa katika maeneo ya kusubiri ndege ya Port of Dover na Eurostar huku watu wakijarubu kuingia kabla ya marufuku ya safari kuanza kutekelezwa.

**BBC**



Wafanyakazi wa kikosi cha uokoaji wakisaidia kuwatafuta watu waliokwama katika mafuriko baada ya kimbunga Rai kuupiga mji wa Cagayan de Oro City, kusini mwa Ufilipino juzi. **PICHA: AP**

# Matumaini yapatikana majadiliano ya nyuklia

**VIENA,** AUSTRIA

WANADIPLOMASIA wa mataifa ya magharibi wamekiri kuwepo kwa hatua fulani latika mazungumzo ya kujaribu kuunusuru mkataba wa nyuklia kati ya Iran na madola yenye nguvu.

Wawakilishi wa Uingereza, Ujerumani na Ufaransa wanaofahamika kama E3, walisema kuna mafanikio fulani ya kiufundi yamepatikana ndani ya saa 24 zilizopita, lakini bado kuna kiwingu cha kukatisha tamaa kutokana na tabia ya Iran.

Miongoni mwa wasiwasi wa mataifa ya magharibi ni kuwa Iran hivi karibuni itakuwa imepiga hatua za kutosha kiuchumi kiasi kwamba mkataba wa nyuklia wa mwaka 2015 uliotoa ahadi ya kulegeza vikwazo vya kiuchumi kwa nchi hiyo ya uajemi utapoteza uzito.

Iran iliomba mapumziko ya muda kwenye mazungumzo hayo ili wanadiplomasia wake wakafanye mashauriano na viongozi wakuu kuhusu mwelekeo wa kuchukua kwenye majadiliano hayo yanayofanyika mjini Vienna.

**DW**

## Ethiopia kuchunguzwa ukiukwaji haki za binadamu

**GENEVA,** USWISI

BARAZA la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, limepiga kura kuunga mkono kuundwa kwa jopo la wataalamu watakao chunguza vitendo vya kukiukwa haki za binadamu katika vita vya nchini Ethiopia vilivyoanza tangu Novemba mwaka jana. Hata hivyo serikali ya Ethiopia imepinga uamuzi huo na kuuelezea kuwa ni wa ukoloni mamboleo.

Kura hiyo ilifanyika kwenye makao makuu ya Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa mjini Geneva nchini Uswisi, katika wakati Naibu Kamishna Mkuu wa haki za binadamu akisema wameendelea kurekodi taarifa za ukiukaji wa haki za watu nchini Ethiopia.

Nchi wanachama 21 ziliunga mkono azimio hilo, 11 hazikushiriki ikiwa ni pamoja na Sudan na Senegal na nchi wanachama 15 zilizilipinga azimio hilo ikiwa pamoja na China na Urusi.

## Kimbunga Rai chaua 19 Ufilipino

**MANILA,** UFILIPINO

KIMBUNGA kikali kilichoipiga Ufilipino juzi kimesababisha vifo vya watu 19,na kuacha maeneo mengi yakiwa yameharibiwa miundombinu ya umeme na kukatisha mawasiliano katika jimbo la katikati mwa nchi hiyo.

Taarifa zilizotolewa na polisi ya nchi hiyo, ilisema watu wengi walipoteza maisha baada ya kuangukiwa na miti iliyong´olewa na upepo mkali.

Tufani hiyo iliyopewa jina la Rai imeelekea katika bahari ya China kusini baada ya kuyapiga pia majimbo ya mashariki mwa Ufilipino ambako zaidi ya watu 300,000 walilazimika kuhamishwa mapema kabla ya kuwasili kwake.

Gavana wa jimbo la kati alisema kimbunga Rai kilichokuwa kinasafiri kwa kasi ya kilometa 195 kwa saa, kimehujumu karibu kila kitu kwenye eneo hilo.

## Watu 24 wateketea kwa moto hospitalini

**OSAKA,** JAPAN

WATU 24 wamekufa nchini Japan kufuatia moto kuteketeza kituo kimoja cha afya kwenye mji wa Osaka.

Hata hivyo, polisi inashuku uliwashwa na mmoja ya wagonjwa kwenye kliniki hiyo.

Shirika la habari la Japan, Kyodo, limeripoti likinukuu duru ya polisi kwamba maofisa wa usalama wanashuku kuwa mwanaume mmoja mwenye umri wa miaka 61 ndiye aliwasha moto huo.

Mwanaume huyo anayeaminika yuko katika hali mahututi kutokana na mkasa huo, ni miongoni mwa majeruhi 27 waliopelekwa hospitali baada ya moto kuiteketeza kabisa kliniki iliyo kwenye ghorofa ya nne.

Kulingana na mashuhuda kwenye kliniki hiyo huenda mtuhumiwa huyo ambaye sasa anachunguzwa na polisi alimwaga kimiminika kutoka kwenye begi lake na kisha kuwasha moto.

**DW**

# SAFU

## MAKALA

# MALUMBANO NI HATARI KWA UMOJA WETU



Na Magabilo Masambu

SIFA kubwa tuliyokuwa nayo kama nchi ilikuwa juu ya umoja wetu. Majirani na dunia walijua hivyo, ndiyo maana wenye shida na nchi zao tulikuwa washauri na wasaidizi wao. Inawezekana bado tu washauri wao lakini nafikiri sasa wanaweza kuwa wanatutazama tofauti.

Tunajenga nchi kwa manufaa yetu sote na vizazi vyetu, hivyo ya nini tugombanie fito? Pengine wakati mwingine kutotambua wapi fito na miti iliyojenga nyumba yetu ilikotoka, linaweza kuwa tatizo. Kuna wakati kutofahamu sawasawa historia ya mafanikio yetu, inaweza kuzaa laana ambayo yaweza kuwa inatufarakanisha bila kujijua.

Kuna umuhimu wa kuwa na mawazo jumuishi.

Nikubaliane na kauli ya Rais Samia Suluhu aliyoitoa wakati wa mkutano na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa hivi karibuni kwamba katika nchi hii hakuna mwenye hati miliki na kwamba tuishi kwa kuheshimu sheria za nchi.

Ukweli huo unapaswa kuheshimiwa na kila mmoja wetu kwa sababu sheria hazipaswi vilevile kusimamiwa kwa kubaguliwa maana tunaambiwa sheria ni msumeno na kwamba unakata pande zote.

Hakuna jambo jema ndugu mnapoona kuna jambo haliendi sawa mkaitana mezani kwa ajili ya mazungumzo.

Sheria nyingi duniani zimetungwa kwa ajili ya wahalifu na hazijawahi kutoa suluhu iliyo njema. Siamini kwamba tunashindwa kuitana na kuzungumza iwe ndani ya vyama vyetu au nje.

Mivutano hii inaweza kutumika kama mifupa anayorushiwa mbwa anayemfukuza mwizi.

Mwisho wa siku mwizi hatakamatwa na badala yake mbwa ataendelea kuzubaa akila mifupa hiyo ambayo pia ataishia kuilambalamba tu kwa sababu hana uwezo wa kuitafuna.

Maana yangu ni kwamba tumetimiza miaka 60 ya uhuru lakini maendeleo tuliyo nayo leo hatuwezi kujivuna sana japo nakubali kwamba yapo mambo yamefanyika katika ujenzi wa miundombinu, elimu, afya na maeneo mengine lakini kusema ukweli pengine tusingekuwa na hii mivutano na malumbano, tungekuwa tumepiga hatua zaidi.

Siku tutakayotambua kwamba kila mmoja katika nchi ana mchango katika maendeleo bila kutazama dini, kabila, chama cha siasa anachotoka na kwamba mawazo na jitihada zake zinatumika na kuheshimika basi tungalikuwa tuko mbali zaidi ya hapa.

Inawezekana tunayo matatizo katika maeneo ya kisheria yatazamwe, kama ni ya kimaadili yazungumzwe ili mradi turudi kama taifa moja lenye nia moja ya kujenga nchi. Bahati mbaya tulio nayo ni kwamba nia njema zinazungumzwa lakini hazitekelezwi.

Yasiyozungumzwa ndiyo hutekelezwa, yasiyotekelezwa ndiyo yanahitajika, wanaoyahitaji hawayazungumzi.

Pengine hajapatikana refa anayetakiwa kupuliza kipenga wakati timu mbili zinapokuwa uwanjani. Ninachoamini ni kwamba kama kuna watu wawili wamekosana au hawaelewani, lazima apatikane mtu wa tatu nje ya mahakama za kisheria badala yake ndani ya mahakama za majadiliano ili kusikiliza hoja za pande mbili na kuwaunganisha wawili hawa.

Zamani kwenye migogoro mingi waliitatua wazee. Bado naamini wazee hao hawajaisha.

Iwe migogoro ya kimila au kichama au kiserikali wanaweza kusimama kwenye nafasi zao wakashauri kwa sababu kuishi kwingi kufahamu mengi.

Inawezekana makosa mengine yanatokana na kutoijua historia ya mambo na tukifahamishwa tunasema aaa alah kumbee na mambo yanakuwa yamekwisha.

Kauli na vitendo ni mambo mbalimbali zinaweza kutoka kauli nzuri sana kwa viongozi wetu juu ya umoja wetu lakini vitendo vikakinzana hilo ni tatizo moja tulilo nalo Afrika.

Hili linatokana na utamaduni wa kufundishwa uongo tukiwa wadogo. Mara nyingi tu inatokea kutoa maelekezo kwa watoto kwamba mtu fulani akija mwambieni sipo nimetoka wakati umelala ndani.

Kwa hiyo mtoto tayari anafundishwa kusema asichoamini hata mwenyewe maana anafahamu fika upo.

Naamini kwamba siku tutakapoamua kuzitendea haki hotuba zetu na matamko mbalimbali tukayatekeleza kama tunavyoyasema hadharani basi tunaweza kuwa tumetengeneza jambo jema ambalo litabaki kwenye historia ya maisha yetu. Mzee Mwinyi amewahi kusema maisha ni hadithi tu basi unapoondoka duniani uache hadithi nzuri.

Hii ni kwa sababu madaraka yana muda mfupi sana na wameshapita wengi ambao walitisha sana enzi zao lakini zimebaki ama historia nzuri ama mbovu.

Bado tunayo nafasi ya kuwa wamoja pamoja na tofauti za vyama. Itikadi si kwa kutangaza kwamba tu wamoja bali kwa vitendo.

Kila mmoja anatakiwa kujiona kuwa anayo nafasi sawa ya kujiletea maendeleo binafsi pamoja na maendeleo ya nchi.

Haipaswi kuonekana kwamba wako wanaotakiwa kujenga nchi na wengine wabaki watazamaji. Hiyo haitakuwa tofauti na ubaguzi wa aina yoyote ile kama wa rangi na kadhalika.

**Mungu ibariki Tanzania.**

**0689157789**

**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kifo 'tata' cha Zengekala kilivyoshtua Wabongo*



Na Adam Fungamwango

ILIKUWA saa 3:00 usiku ya Desemba 17, 1987 kwenye kipindi cha Majira cha Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) ndipo mtangazaji alipowatangazia Watanzania kifo cha ghafla cha mwanamuziki maarufu wakati huo, Nico Zengekala.

Kilichotokea ni taharuki. Hakuna aliyeamini kuwa Nico, mwimbaji mwenye sauti tamu, nyororo ambaye ni mwenye ulemavu wa macho, amefariki dunia. Ni mwanamuziki ambaye alikuwa ameshajinyakulia mashabiki wengi nchini Tanzania, miaka michache tu tangu aingie nchini kutokana na umahiri wake wa kuimba, akitokea kwao Kenya.

Habari zaidi zinasema kuwa hadi saa 6:00 usiku wa kuamkia kifo chake, alikuwa anapiga soga na marafiki zake mitaa ya nyumbani kwake, Kariakoo mtaa wa Sikukuu, jijini Dar es Salaam ambako alipewa nyumba ya kuishi na bendi aliyokuwamo ya Juwata Jazz, wana Msondo Ngoma. Nyumba hiyo ilikuwa moja ya zile zilizokuwa zinamilikiwa na JUWATA.

Ijumaa iliyopita, ilitimu miaka 34 tangu Afrika Mashariki ilipompoteza mwimbaji kijana, aliyefariki dunia ghafla kwa kile madaktari walichosema kuwa ni ugonjwa wa kifafa. Alifariki dunia akiwa na umri kati ya miaka 20 na 24.

Kutokana na ustaa wake na kifo chake cha ghafla, ilisababisha taharuki kubwa, vilio, simanzi na kila aina ya huzuni Tanzania, Kenya na Uganda huku baadhi ya Wabongo wakiwa hawaamini kama kilikuwa kifo cha kawaida.

Ni kifo kilichozua maneno mengi kuliko kawaida. Wengine wakasema ni mambo ya kishirikina. Wako waliodai alilishwa sumu na wengine walisema umaarufu wake alioupata kwa muda mfupi tu, ulikuwa mwiba kwa wanamuziki si wa Msondo tu, bali hata wa Tanzania nzima.

Alionekana kuwafunika, hivyo baadhi yao hawakupendezewa. Lakini yote hayo yanamalizwa na ripoti ya madaktari kuwa alifariki dunia kwa ugonjwa wa kifafa. Alipoingia nchini na bendi ya Les Cubano, alitamba na vibao kama 'Jackie', 'Mwalimu Nyerere', 'Suzzy', 'Bwana Salim', 'Shemango' na 'Mama Hisani'..

Mwaka 1985 alichukuliwa na Msondo Ngoma ambako nako alitamba na vibao kama 'Solemba' alichokitunga mwenyewe na vingine akiviimba kwa ustadi mkubwa kama 'Hasira Hasara', 'Kaka Mahmood', 'Asha Mwanasefu', 'Priscilla' na 'Kambarage Nyerere'.

Wengi hawajui kuwa Zengekala aliimba kwa umahiri mkubwa na kutunga nyimbo ambazo hadi anafariki dunia alikuwa hajazirekodi. Nazo ni 'Dalila', huku akitunga 'Cha Mlevi Huliwa na Mgema', pamoja na 'Razole' ambazo kama angebahatika kurekodi ingekuwa habari nyingine.

Wimbo wa 'Tabu Mpaka Lini' ambao umerekodiwa, kuna baadhi ya vipande aliimba Nico na alipofariki dunia, wakati wa kurekodi viliimbwa na watu wengine.

Ni kile kilichoimbwa na Suleiman Mbwembwe "Bwana eee, ooh bwana ee, tabu hii mpaka lini jamani.", na kingine alichoimba Tino Masinge "Sikia eee, makosa tuliyoyafanya awali we mama tukifanya tena marafiki watatucheka." Hivi vyote awali ilikuwa virekodiwe na Nico, lakini alifariki dunia kabla ya kwenda studio.

Alikuwa na sauti tamu, nyororo, kali, ambayo alikuwa na uwezo wa kuitetemesha na kusikika kama maporomoko ya maji, wakati mwingine akiishusha sauti kama mtu anayeweweseka hivi.

Alizaliwa katika kijiji cha Wundayi eneo la Mwatate karibu na mji wa Voi, kilometa kiasi cha 100 hivi kutoka Mombasa nchini Kenya.

Alichukuliwa na kuletwa nchini na mabaki ya wanamuziki wa Super Volcano ya Mbaraka Mwinshehe aliyefariki dunia Kenya mwaka 1979, Simba Wanyika, Les Wanyika, Wanyika Stars, Super Wanyika na Jobiso, ambao walimwona akiimba kwenye bendi moja ya Wataita wenzake Nairobi.

Wanamuziki hao ambao ni Watanzania waliokuwa nchini humo wakiendelea na shughuli za muziki, waliombwa kurejea nchini na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro wakati huo, Nicodemus Banduka, hivyo wakaamua kumchukua Nico ambaye pia alitaka kuondoka Kenya.

Kwa mujibu wa mwanamuziki Said Makelele ni kwamba ilibidi kwenda kumwomba baba yake, ambaye aliwakubalia kwa madai kijana wake ameshindikana kwa kuwa amemkataza sana mambo ya muziki lakini amekuwa akitoroka nyumbani na kwenda kuimba sehemu mbalimbali.

Makelele anasema ilibidi wadanganye ni Mtanzania ili aruhusiwe kuvuka mpaka wa Tanzania na Kenya kwani wakati huo alikuwa na umri wa miaka 17, hivyo asingeweza kuruhusiwa kuvuka. Walidai ni Mtanzania wa Dodoma na wao ni wanamuziki wanaorejea nyumbani Tanzania kwa wito wa Mkuu wa mkoa wa Morogoro, ndipo waliporuhusiwa.

Inawezekana wakati anafariki dunia huenda alikuwa hajafikisha miaka 24 na inawezekana Msondo walimpandisha umri ili aajiriwe na Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania (JUWATA) kwani wasingeweza kumuajiri mtoto.

Kama aliingia nchini ana miaka 17 na hakudumu na bendi hiyo kwa zaidi ya miaka miwili akajiunga na Msondo. Ni mwanamuziki aliyedumu kwa muda mfupi nchini, lakini sauti na uimbaji wake hadi leo umeendelea kuwa lulu na wimbo wake wa 'Solemba' na msamiati ukiendelea kuishi.

Hakuwa staa kwao Kenya, lakini nyota ilimuwakia nchini na hata mwili wake uliposafirishwa, ulikuwa ni msafara na heshima kubwa wa magari lukuki ya serikali ya Tanzania, JUWATA, Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania (CHAMUDATA), wapenzi na mashabiki kama vile anayekwenda kuzikwa ni kiongozi mkubwa wa kitaifa.

Hii iliwashangaza na kuwaliza wengi kwao, zaidi wazazi na ndugu zake, kwani aliondoka akiwa wa kawaida tu lakini maiti yake imerudishwa nyumbani kishujaa. Hakuamini.

Alizikwa kijiji kwao Wundayi, Mwatate, Voi, Taveta nchini Kenya Desemba 24, 1987.

# HADITHI

# Ajenda ya siri-9

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

EEEE shoga, na mikate juu."

"Bibi weee yatakushinda, yaani umeshapekua na kuona mikate?"

"Si ulimjibu vibaya kaka wa watu mwanzo wewe, tena sema yule hana hasira, ingekuwa mwingine mngekorofishana, lakini kaenda na wewe taratibu hadi kakunasa."

Fatuma alikuwa akimpasha mwenzake.

"Wapi, hajaninasa wala nini?"

"Yaani unanifanya mimi mtoto mdogo, vile vicheko vya ndani ofisini vilikuwa vya kawaida vile. Tofauti ni lile jicho ulilokuwa unamuangalia mwanzo alipokuja hapa na kuuliza maswali."

"Da Fatu, humjui yote, anachekesha. Yaani ni mcheshi, ukikaa naye yule utakuwa unafurahi tu."

"Ndiyo maana naona baada ya kuja yule kaka, umekuwa na furaha sasa. Haya sisi tupo tutayaona."

*******************************


Aliamka akiwa mchovu kidogo. Alianza kukumbuka safari yake aliyoifanya siku nne zilizopita. Alikumbuka awamu yake ya kwanza ya kazi ya kujua usahihi wa hukumu ya Tina, ulimpeleka hadi Tegeta, akakutana na mrembo Mwahija, mtoto wa Tanga. Akakumbuka pia alipokuwa anampeleka kwenye nyumba aliyokuwa anafanya kazi msichana huyo alipiga picha nyumba na eneo la marehemu Hafidh Chilambo kwa kutumia simu yake ya mkononi.

Pamoja na kwamba alikuwa na njaa pia, ukiondoa uchovu, lakini aliamua kukaa kwanza kuangalia picha ambayo alipiga kwenye nyumba hiyo na mandhari yake kwa uangalifu.

Zilikuwa picha mbili. Moja ilikuwa jumba la kifahari la marehemu. Ya pili ambayo aliipiga akiwa katikati ya geti ilionyesha madhari ya ndani kwa sababu geti lenyewe halikuwa lile linaloficha ndani, bali lilikuwa fupi kwa kwenda juu, halafu lilinakshiwa zaidi na nondo kuliko mabati, au mbao za kuziba ili ndani kusionekane.

Ilionyesha bustani nzuri iliyokuwa mbele ya nyumba hiyo ya kisasa. Pembeni kulikuwa na magari mawili. Moja ni Toyota Harrier la rangi ya kijivu na nyingine ni Toyota Alphard ya rangi nyeupe.

Kwa kawaida haikuonekana ya maana, lakini kwake kama mpelelezi aliona ni mwanzo mzuri wa kuanza au kutaka kujua kila kitu kwenye nyumba hiyo, kabla ya kusonga mbele. Akakumbuka msemo unaosema ukitaka kutafuta nyoka usiku kwa kutumia taa, anzia miguuni mwako.




**"Mimi naitwa Mzee Mwayangu, kote huku najulikana, hakuna ambaye hanifahamu na nyumba yangu haiko mbali sana na hapa. mwenzangu unatokea wapi?**

Katika sakata hili alitaka aanze kwanza kujua ni nani anaishi mle ndani kwa sasa baada ya Chilambo kufariki dunia. Ni mke wa marehemu na watoto wake au nao wameondoka? Wamepangisha nyumba au wameuza?

Akakumbuka kuna baadhi ya familia za wanamume huwatimua wanawake kwenye nyumba baada ya waume zao kufariki dunia, hivyo alitaka kuanza na hilo.

Baada ya kupumzika kwa siku tatu akifanya kazi zingine, aliamua siku ya leo kuendelea na kazi aliyojipa.

Aliamua kwenda tena Tegeta. Safari hii hakutaka kwenda na gari na wala hakutaka kwenye duka la madawa kwa kina Mwahija. Kuna kitu alikiona siku ile alipokuwa akitembea kwa miguu na Mwahija.

Kutoka Kijitonyama nyumbani kwake kwenda Tegeta, aliamua kupanda daladala. Kwanza alihakikisha anajibadilisha mwonekano. Hakujitofautisha sana na siku ile ila alivaa kapelo moja kubwa ambayo ilimfanya sura yake isionekane kwa asilimia kubwa. Akavaa pia miwani ya jua. Nia ilikuwa ni kutojulikana na yoyote yule ambaye alimuona siku nne zilizopita na kumhisi, hata kama ni Mwahija.

****************************

Safari ilimpeleka moja kwa moja kwa mzee mmoja anayeonekana kuelekea kwenye miaka 70 hivi. Hakuna mita nyingi sana kutoka kwenye duka la dawa la kina Mwahija. Mzee huyo alikuwa akifanya biashara ambayo ilishangaza kidogo. Kuna baadhi ya wazee wa mjini ambao wana biashara ambazo mtu mwingine hawezi kuzifanya.

Alikuwa akiuza miswaki ya miti isiyozidi 10. Nyanya chungu ambazo zilionekana kwa hesabu ya haraka haraka kama nane hivi. bamia mafungu matatu, samaki aina ya nguru na papa ambao wamekaushwa na kutiwa chumvi nyingi ambao walikatwakatwa vipande vidogo vidogo visivyozidi 13.

Kwa ujumla, bidhaa zilikuwa chache mno kuliko meza yake. Alikuwa amejenga kibanda chake kwa kutumia mabati makuukuu, vipande vya mbao, meza iliyokuwa imesimamishwa na miti.

Alipofika karibu yake alimwamkia "Shikamoo mzee."

Mzee huyo alimtazama kwanza, sura yake ilionyesha mshangao kidogo kwani alionekana ni mgeni hapo, na huenda hakuonekana kama ni mteja anayeweza kununua chochote anachouza hapo.

"Marahaba kijana, hujambo?"

"Sijambo, samahani mzee."

"Bila samahani kijana."

"Kidogo nina mazungumzo na wewe kama dakika tano au kumi hivi, naomba univumilie mzee." Alisita kidogo na kuzidi kumwangalia mgeni huyo wa ajabu.

"Mazungumzo gani kijana?"

"Ya kawaida tu, mimi ni mgeni hapa kwa hiyo kuna vitu nataka kuuliza ili nielekezwe."

"Ahaa basi kaa kwenye hapo."

Mwenyewe alikuwa amekaa kwenye kitu cha marimba. Lakini pembeni yake kulikuwa na gogo la mnazi ambalo inaonekana mtu au watu wanaokuja hapo huwa wanakaa.

Eddy alikaa kwenye gogo la mnazi. Akaingiza mfukoni na kutoa noti ya shilingi elfu kumi.

"Najua nitakupotezea dakika kadhaa, kwa hiyo nafidia muda wako, utapata soda baadaye." Alisema huku akimpa noti moja ya thamani ya pesa hiyo.

Mzee aliendelea kushangaa, lakini alipokea na kuiweka kwenye mfuko wa koti lake. Kwake ilikuwa pesa nyingi sana ambayo hakufikiria kuipata ghafla na bila sababu yoyote siku ile. Sasa alionekana kuchangamka.

"Mimi naitwa Mzee Mwayangu, kote huku najulikana, hakuna ambaye hanifahamu na nyumba yangu haiko mbali sana na hapa. mwenzangu unatokea wapi?"

"Mzee mimi natoka mbali sana. Kwanza samahani, maana maswali yangu unaweza ukayaona kama ya kipuuzi hivi."

"Maswali gani hayo?"

"Kwanza mimi ni mjomba wa msichana mmoja anaitwa Tina, ambaye kama una kumbukumbu vizuri alihukumiwa kunyongwa hadi kufa kutokana na kumuua tajiri yake."

"Huyu jamaa wa pale mbele aliyewekewa sumu kwenye chakula?"

"Ndiyo huyo huyo mzee."

"Duh, pole sana, wewe ndiye mjomba wake?"

"Ndiyo." Alijibu na moja kwa moja akaanza kuingiza maswali aliyotaka kumuuliza.

"Hivi mpwa wangu unamfahamu?"

"Haa, yule msichana, si alikuwa anapita hapa tena namtania mchumba wangu. Hawezi kupita hapa bila kunisalimia. Tena akipita hapa alikuwa ujue anakwenda dula la dawa hapo."

"Ina maana mzee kumbe si mara ya kwanza kununua dawa kwenye duka lile?"

"Yaani ndiyo duka lake. Hata yeye mwenyewe akiumwa, ananiambia babu leo kichwa kinauma, nakwenda kununua dawa. Pole sana kwa yaliyompata mpwao, sasa unachohitaji hapo ni nini? Kwenda kule kwa tajiri yake?"

"Ndiyo, kuna vitu ameviacha kule ya muhimu sana, lakini kabla sijaenda ni lazima nijue nakwenda vipi, nisije nikafukuzwa au kugeuziwa kibao na familia ya marehemu."

"Kweli kabisa kijana, ila mimi nitakusaidia kama unataka kwenda."

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# JOHN NINI KUTUA BONGO

MSANII wa kizazi kipya kutoka nchini Denmark, Jonathan Nininahazwe, maarufu kama John Nini, anatarajia kutua Tanzania mapema mwakani katika ziara maalum ya kimuziki.

Akizungumza na Nipashe, John Nini ambaye anatamba na wimbo wake 'Iza Bella', amesema huo ni ujio wake wa kwanza hapa nchini na atafurahi kukutana na mashabiki wake.

" Nimeshapata uhakika sasa nitakuja Tanzania Februari, mwakani nitakuja kuonana na watu wangu na kufurahia utamaduni wa kitanzania na nitafungua milango ya kolabo na wasanii wakubwa hapo Bongo," amesema John Nini.



# JAY Z

## ANUNUA SAA BIL. 14

HIVI karibuni mwanamuziki wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, aliibua maswali mengi pale aliponunua saa ya mkononi kwa milioni 600, lakini alichokifanya rapa Jay Z, utagundua kumbe diamond hakufanya kitu.

Taarifa zinasema Jay Z ameamua kuishangaza dunia pale alipoonekana akiwa na saa mpya ya mkononi aina ya 'Patek Philippe Tiffany Blue Nautilus 5711' yenye thamani ya Dola Milioni 6.5 sawa na shilingi bilioni 14.

Saa hiyo ambayo inatajwa kuwa na gharama kubwa duniani, ameonekana nayo siku za hivi karibuni wakati anaitangaza filamu yake ya The Harder They Fall kupitia mtandao wa Netflix.

# Mwakajila unapotoka Ki-Nigeria

MWIMBAJI wa Injili anayewakilisha vyema Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mwakajila, amekuja kivingine baada ya kutambulisha wimbo wake mpya 'My Story' wenye vionjo kutoka Nigeria.

Mwakajila ameliambia Nipashe hivi karibuni kwamba ameamua kuja na ubunifu huo ili kuwa tofauti na waimbaji wengine na pia kuwasilisha vizuri ujumbe uliopo ndani ya wimbo huo.

"Muda wowote kutoka sasa nitaachia audio na video ya 'My Story', ni wimbo mzuri ambao utapendwa na watu wote sababu umebeba ushuhuda wa maisha yangu na jinsi Mungu alivyonipigania wakati natoka Kilimanjaro kuja hapa Dar es Salaam," amesema Mwakajila.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RASHFORD AITAKA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 24 yuko tayari kusaini mkataba na Barcelona. ***(Sport)***

### MARTIAL NJIA MOJA

NYOTA wa Manchester United na Ufaransa, Anthony Martial, mwenye umri wa miaka 26, anataka kuondoka hapo Old Trafford haraka iwezekanavyo, amesema wakala wake. ***(Manchester Evening News)***

### MARTIAL ANUKIA JUVE

ANTHONY Martial anaweza kujiunga na Juventus Januari kwa mkataba wa mkopo hadi mwisho wa msimu. ***(Sun)***

### PHILLIPS AWEKWA SOKONI

LIVERPOOL wametangaza thamani ya mlinzi wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Nat Phillips, mwenye umri wa miaka 24 kuwa ni pauni milioni 15. ***(Athletic)***

### MARTIAL ATAJWA NEWCASTLE

WAMILIKI wa klabu ya Newcastle United wameshauriwa kumsajili, Anthony Martial ili kuboresha kikosi chao. ***(Transfer Window Podcast)***

### PHILLIPS ANUKIA DYNAMO

EVERTON wamefikia makubaliano na Dynamo Kyiv ya kusaini mkataba na mlinzi wa kati, Nat Phillips mwenye umri wa miaka 24, kwa malipo ya pauni milioni 18. ***(Mail)***

### XAVI AMTAKA TORRES

MSHAMBULIAJI wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Hispania, Ferran Torres (21), ni mchezaji namba moja anayelengwa na kocha wa Barcelona, Xavi wakati kitakapofika kipindi cha uhamisho wa wachezaji cha dirisha dogo la Januari. ***(Sport)***

### BARDGHJI AGOMBEWA ULAYA

CHELSEA, Barcelona, Bayern Munich na Ajax zote zimewatuma mawakala wake katika klabu ya FC Copenhagen kumwinda kiungo wa kati na raia wa Sweden, Roony Bardghji, mwenye umri wa miaka 16. ***(Goal)***

### MELO ATAKIWA ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anamwania kiungo wa kati wa Juventus na Timu ya Taifa Brazil, Arthur Melo, mwenye umri wa miaka 25. ***(FourFourTwo)***

### SWIFT AIKATAA LEEDS

KLABU ya Leeds United imepata pigo katika juhudi zake za uhamisho wa wachezaji Januari baada ya kiungo wa kati, John Swift mwenye umri wa miaka 26, kusema anataka kuendelea kubakia Reading. ***(Reading Chronicle)***

### EVERTON YAJIPANGA

EVERTON wana nia ya kumsajili beki wa kushoto wa Dynamo Kiev na Timu ya Taifa ya Ukraine, Vitaliy Mykolenko mwenye umri wa miaka 25 kwa pauni milioni 20. ***(Liverpool Echo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI: WACHEZAJI BARCA HAWAIELEWI STAILI YANGU

**Aeleza bado wana nafasi ya kupambana na kumaliza msimu ndani ya...**

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Xavi amedai baadhi ya wachezaji wake "hawaelewi" staili yake ya uchezaji ambayo ameianzisha.

Akiwa ameteuliwa kuchukua mikoba ya, Ronald Koeman, kiungo huyo wa zamani amekuwa na mwanzo mgumu pale Camp Nou kwa timu kutokuwa katika kiwango cha kuvutia.

Barca imeshinda mechi mbili tu kati ya sita tangu Xavi amerudi klabuni hapo, huku sare ya bila kufungana dhidi ya Benfica na kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Bayern Munich kuliwashuhudia wakishindwa kufuzu hatua ya 16 kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 20.

Kabla ya mchezo wa jana Jumamosi dhidi ya Elche, miamba hao wa Katalunya walikuwa katika nafasi ya nane kwenye msimamo, wakipitwa pointi 18 na vinara wa LaLiga, Real Madrid.

Na sasa Xavi amesema tatizo lipo kwa wachezaji wake ambao wameshindwa kuendana na staili yake anayoitaka wacheze.

"Sisi ni Barca na tunatakiwa kushindana na wapinzani wetu bila kujali tuna majeruhi au la. Hatutakiwi kutoa sababu.

"Malengo yetu ni kuwa kwenye nne bora na kushinda mataji, ingawa tofauti kati yetu na vinara ni kubwa sana. Hatuwezi kupinga chochote.

"Tunatakiwa kuelewa namna soka inavyotakiwa kuchezwa. Inashangaza namna wachezaji wa Barca wanavyoshindwa kuendana na staili yangu."

CHEZA USHINDE KASINO

MECHI KALI
HOME AWAY
TOTTENHAM
5.01 | 4.31 | 1.59
LIVERPOOL

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CONTE ASEMA SALAH NI BORA DUNIANI




**LONDON, England**

ANTONIO Conte amemtaja, Mohamed Salah kuwa "mmoja wachezaji bora duniani" kuelekea mchezo wa Ligi Kuu England kati ya Tottenham Hotspur dhidi ya Liverpool, leo Jumapili.

Liverpool imepitwa pointi moja na vinara wa ligi hiyo, Manchester City, huku Salah akiwa kwenye kiwango bora kukiongoza kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri alifunga wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Newcastle United Alhamisi iliyopita, akifikia rekodi ya Jamie Vardy kwenye Ligi Kuu England kwa kufunga au kutoa asisti katika mechi 15 mfululizo.

Salah amehusika kwenye mabao 24 katika Ligi Kuu England msimu huu (akifunga mabao 15 na asisti tisa), akiwa amepitwa na straika wa zamani wa Newcastle, Alan Shearer, pekee aliyefunga mabao 16 na asisti tisa kwenye ligi hiyo kabla ya Krismasi akifanya hivyo msimu wa 1994-95.

Na Conte amesema Salah ambaye ni mchezaji wa zamani wa AS Roma akiwa na umri wa miaka 29, ni nyota mwenye ubora wa hali ya juu sana.

"Nafikiri yeye ni mmoja wa wachezaji bora duniani kwa sasa," alisema Conte akiwaambia waandishi wa habari kuhusu Salah.

"Katika mchezo huo tumeona namna gani anavyofunga na kutoa asisti. Ni mchezaji mwenye maamuzi.

"Mara zote anapokuwa na mpira ni hatari, ameimarika sana, namkumbuka wakati akicheza nchini Italia."

# Eriksen amalizana rasmi na Inter



**MILAN, Italia**

INTER Milan imethibitisha kuachana na aliyekuwa mchezaji wa klabu hiyo, Christian Eriksen.

Hayo yamekuwa ni maridhiano baina ya pande zote mbili na sasa yupo huru kusajiliwa timu nyingine yoyote.

Eriksen amekuwa nje ya uwanja kwa muda tangu alipopata matatizo ya moyo akiwa kwenye majukumu ya timu ya taifa kwenye mashindano ya Euro 2020.

Baada ya tatizo hilo kutokea, Eriksen aliwekewa mashine katika mfumo wake wa moyo.

Kwa mujibu wa sheria za Ligi Kuu Italia, Serie A, hairuhusiwi mchezaji mwenye matatizo kama hayo kucheza katika ligi hiyo na hivyo, Inter pamoja na Eriksen, wamefikia makubaliano ya kukatisha mkataba.

Baada ya kusitisha mkataba wa Eriksen, mchezaji huyo sasa yupo huru kuamua klabu nyingine atakayoitumikia nje ya Serie A.

LIVE IN PLAY

# BIASHARA YAIITA YANGA MEZANI

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Biashara United umesema uko tayari kumwachia winga, Denis Nkane ili kujiunga na Yanga au timu nyingine yoyote inayomhitaji endapo watafuata taratibu za uhamisho wa usajili wa nyota huyo.

Biashara United bado ina mkataba na winga huyo ambaye ameonyesha kiwango kizuri tangu kuanza kwa msimu huu wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho ambayo timu hiyo ilishiriki.

Kauli hiyo ya Biashara imekuja kutokana na kuwapo kwa tetesi za Yanga kuhitaji huduma ya Nkane na tayari inaelezwa wameshapeleka ofa ya mkataba wa miaka miwili.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso, alisema bado hawajapokea barua rasmi kutoka Yanga lakini wamefungua milango ya kumuuza nyota huyo.

"Ni kweli tumeona hizo taarifa kwenye mitandao ya kijamii, lakini hatujapokea barua rasmi kutoka Yanga, kama wanahitaji mchezaji wetu na watakuja kuzungumza, hatuwezi kuwakatalia kwa sababu soka ni biashara na ajira kwa sasa," alisema Mataso.

Aliongeza tayari wamefanya kikao na benchi la ufundi la timu hiyo lililoko chini ya Kocha Mkuu, Patrick Odhiambo kwa ajili ya kujadili mchakato wa usajili wa nyota wapya kwenye dirisha dogo ili kuongeza nguvu na kuimarisha kikosi chao.

Matoso alisema malengo ya timu hiyo ni kuhakikisha wanafanya vizuri katika mechi za ligi na hatimaye kupata tiketi ya kushiriki katika mashindano ya kimataifa mwakani.




Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Oscar Mirambo (kulia), akimkabidhi mipira ya aina mbalimbali Mratibu wa East African Chipukizi Cup, Alfred Itael kwa ajili ya kuendeleza soka katika kituo chake. **PICHA: TFF**

# Mtaka aikumbusha TOC 'ulezi'

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameiagiza Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), kuwasaidia wachezaji chipukizi wa hapa nchini ili wajitambue na kupanga mikakati kwa ajili ya ushiriki wa mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Mtaka alisema hayo wakati akifungua Mkutano Mkuu wa TOC uliofanyika jijini Dodoma kwa kushirikisha wanachama wake mbalimbali.

Mtaka alisema wanariadha wengi wa Tanzania hawajitambui, hivyo wanahitaji msaada kutoka kwa wakongwe ambao tayari walishiriki mashindano ya kimataifa na kupata mafanikio.

"Unakuta mashindano ya riadha yanaandaliwa hapa nchini lakini mwanariadha hashiriki, zawadi inatolewa Sh. milioni nne kwa mshindi lakini mwanariadha huyo anakwenda kushiriki nje analipwa Sh. milioni 1.4, kitu ambacho ni hasara," alisema Mtaka.

Alisema lengo la serikali ni kuona wanariadha wanafanya 'vitu vya maana' na si kukurupuka kama wanavyokimbilia kwenda nje ya nchi kushiriki mashindano ambayo hayana maslahi kwao.

Naye Makamu Mwenyekiti wa TOC, Henry Tandau, alimshukuru kiongozi huyo kwa kutoa ushirikiano na wanamichezo na kusema wakati wote amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha michezo inasonga mbele hapa nchini.


SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 19 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4208 | Fiorentina vs Sassuolo | 1.86 | 3.94 | 3.74 |
| 15:30 | 1635 | Hannover vs Werder Bremen | 3.44 | 3.39 | 2.02 |
| 15:30 | 1968 | Brugge vs Anderlecht | 1.88 | 3.64 | 3.74 |
| 15:30 | 2462 | Vietnam vs Cambodia | 1.01 | 11.47 | 38.24 |
| 15:30 | 5046 | Malaysia vs Indonesia | 2.71 | 3.15 | 2.42 |
| 16:00 | 3573 | Bursaspor vs Bandirmaspor | 2.54 | 3.26 | 2.50 |
| 16:00 | 3619 | Olympiakos vs Lamia | 1.17 | 6.91 | 13.83 |
| 16:00 | 4387 | Granada vs Mallorca | 2.49 | 3.11 | 2.96 |
| 16:30 | 4828 | Feyenoord vs Ajax | 3.87 | 3.87 | 1.77 |
| 17:00 | 1212 | FK Vozdovac vs Metalac | 1.63 | 3.61 | 4.81 |
| 17:00 | 2292 | Teplice vs Mlada Boleslav | 3.70 | 3.70 | 1.93 |
| 17:00 | 2343 | Wolverhampton vs Chelsea | 6.00 | 3.90 | 1.57 |
| 17:00 | 3927 | Sigma Olomouc vs Zlin | 1.92 | 3.59 | 3.84 |
| 17:00 | 4628 | CFR Cluj vs Argesul Pitesti | 1.50 | 3.78 | 6.68 |
| 17:00 | 5692 | Spezia vs Empoli | 2.62 | 3.57 | 2.51 |
| 17:15 | 5413 | Newcastle vs Manchester City | 12.32 | 6.33 | 1.22 |
| 17:30 | 3529 | SC Freiburg vs Bayer Leverkusen | 2.69 | 3.53 | 2.44 |
| 18:00 | 2233 | Hibernian vs Celtic | 5.02 | 3.96 | 1.54 |
| 18:00 | 3764 | Zaragoza vs Tenerife | 2.40 | 2.95 | 3.09 |
| 18:00 | 4941 | Eupen vs Charleroi | 2.71 | 3.40 | 2.43 |
| 18:15 | 3137 | Athletic Bilbao vs Betis | 2.06 | 3.34 | 3.64 |
| 18:30 | 2961 | FC Sion vs Lausanne-Sport | 2.24 | 3.56 | 2.87 |
| 18:30 | 5177 | FC Basel vs Grasshoppers | 1.77 | 3.79 | 4.04 |
| 18:45 | 5322 | Waalwick vs PSV Eindhoven | 9.83 | 6.09 | 1.23 |
| 19:00 | 5228 | Fenerbahce vs Besiktas | 2.21 | 3.44 | 3.00 |
| 19:00 | 5590 | Maritzburg Utd vs Chippa Utd | 2.04 | 3.05 | 3.84 |
| 19:00 | 5923 | MSK Zilina vs Slovan Bratislava | 3.14 | 3.62 | 1.98 |
| 19:30 | 2830 | Legia Warszawa vs Radomiak Radom | 1.97 | 3.24 | 3.53 |
| 19:30 | 4528 | Hajduk Split vs NK Osijek | 2.02 | 3.33 | 3.28 |
| 19:30 | 4858 | Tottenham vs Liverpool | 5.01 | 4.31 | 1.59 |
| 19:30 | 5100 | FC Koln vs Stuttgart | 2.01 | 3.73 | 3.33 |
| 20:00 | 1655 | Balzan Youths vs Valletta | 2.50 | 3.26 | 2.54 |
| 20:00 | 2483 | Torino vs Verona | 2.22 | 3.35 | 3.20 |
| 20:00 | 2663 | Banik Ostrava vs Slavia Prague | 4.41 | 3.71 | 1.77 |
| 20:00 | 3563 | Benfica vs Maritimo | 1.12 | 7.68 | 18.70 |
| 20:00 | 4451 | Sampdoria vs Venezia | 1.79 | 3.80 | 4.20 |
| 20:15 | 1006 | Huesca vs Alcorcon | 1.74 | 3.43 | 4.71 |
| 20:20 | 1797 | Cholet vs Nice | 8.47 | 5.32 | 1.30 |
| 20:30 | 3246 | Getafe vs Osasuna | 2.46 | 2.90 | 3.25 |
| 20:30 | 3748 | PAOK vs Asteras Tripolis | 1.47 | 4.14 | 6.51 |
| 20:30 | 3823 | Benevento vs Monza | 2.03 | 3.29 | 3.53 |
| 20:30 | 5278 | Panathinaikos vs PAS Giannina | 1.66 | 3.60 | 5.13 |
| 20:30 | 5544 | Racing Genk vs Royal Antwerp | 1.97 | 3.61 | 3.46 |
| 20:45 | 4972 | Zalaegerszegi TE vs Ujpest FC | 2.55 | 3.46 | 2.39 |
| 21:30 | 3621 | Sepsi Osk vs Steaua Bucuresti | 2.95 | 3.15 | 2.36 |
| 22:00 | 1927 | FC Vizela vs Porto | 8.44 | 5.10 | 1.31 |
| 22:45 | 1372 | AC Milan vs Napoli | 2.26 | 3.45 | 3.05 |
| 23:00 | 2035 | Real Madrid vs Cadiz CF | 1.29 | 5.65 | 9.10 |
| 23:00 | 5201 | OH Leuven vs Standard Liege | 2.47 | 3.40 | 2.66 |
| 23:10 | 1206 | Entente Feignies Aulnoye vs Paris St Germain | 41.01 | 12.99 | 1.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumapili Desemba 19, 2021

Nipashe




Xavi: Wachezaji Barca hawaielewi staili yangu

HABARI UK 21

# YANGA YAJIPANGA KUENDELEZA DOZI

## ●●●Lakini Prisons waahidi wako tayari ‘kuvunja mwiko’ kwa vinara hao...

**Na Saada Akida**

KAZI iendelee. Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi kuelekea mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya ‘Maafande’ wa Prisons itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nelson Mandela uliopo Sumbawanga, mkoani Rukwa.

Katika mchezo huo wa raundi ya tisa, Yanga itaendelea kuwakosa wachezaji wake wa kikosi cha kwanza akiwamo Yacouba Songne ambaye ni majeruhi wa muda mrefu, Fiston Mayele, Kibwana Shomari na Yusuph Athuman, ambao pia ni majeruhi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema anatarajia mchezo huo utakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila timu inahitaji matokeo chanya ili kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo ya juu nchini.

Nabi alisema wamejipanga kupambana ili kuhakikisha wanavuna pointi zote tatu lakini pia hawataki kuona nyavu zao zinatikiswa.

“Kila mchezaji yuko tayari kwa mchezo huu, tumejiandaa kutafuta matokeo mazuri katika mechi hii kama tulivyofanya kwenye michezo iliyotangulia, tunajua haitakuwa mechi rahisi kwa sababu tunakutana na timu ngumu, yenye wachezaji wazuri na wenye uzoefu,” Nabi alisema.

Kocha huyo aliongeza kila mechi kwao ni sawa na fainali na wanajipanga kusaka ushindi ili kuendelea kujiimarisha kwenye uongozi wa ligi.

“Ili tufikie malengo yetu ni lazima tupate ushindi katika kila mchezo, tumekuja ugenini, lakini wachezaji wanafahamiana, hivyo tumejiandaa kukutana na ushindani katika dakika zote 90,” alisema kocha huyo.

Aliongeza licha ya kutokuwepo kwa wachezaji wake wanne nyota, amewaandaa wachezaji wengine ‘kubeba’ majukumu ya kuisaidia timu na anaamini watafanya vyema.

“Ligi imekuwa na ushindani mkubwa na kila mmoja anahitaji kushinda mechi zake, Tanzania Prisons ni timu ngumu na tunaenda kupambana nao ili kutafuta pointi muhimu katika mchezo huo, lengo ni kuona tunajiimarisha zaidi katika nafasi tuliyokuwa nayo,” alisema Nabi.

“Kikosi chetu hakijaathirika kutokana na baadhi ya wachezaji kuwa majeruhi, Yanga ina wachezaji wengi na waliobakia watapambana kupata matokeo mazuri katika mechi ya kesho (leo), tuko tayari kwa mchezo,” aliongeza kocha huyo.

Naye Kocha Msaidizi wa Prisons, Shabani Kazumba, aliliambia gazeti hili kikosi chake kimejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na kipo tayari ‘kuvunja mwiko’ kwa kuwa timu ya kwanza kuifunga Yanga msimu huu.

Kazumba alisema ‘wamewasoma’ vyema wapinzani wao kupitia mechi iliyopita walipokutana na Ihefu SC katika michuano ya Kombe la FA na kufanyia kazi ubora na udhaifu wao, hivyo wamejipanga kuona wanaondoka na pointi tatu.

“Licha ya kutopoteza mchezo na kuongoza ligi, hatuna presha nao wala kuwaogopa zaidi, tutaingia uwanjani kwa kuwaheshimu na kuzingatia tunahitaji kubakiza alama tatu katika Uwanja wa Nelson Mandela,” alisema Kazumba.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena kesho kwa Biashara United kuwakaribisha Coastal Union kwenye Uwanja wa Karume ulioko Musoma, Mara.

**TUKO TAYARI**




Wachezaji wa Yanga, Khalid Aucho (kulia) na Heritier Makambo wakiwa katika picha ya pamoja wakati timu yao ikielekea Sumbawanga kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Prisons itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nelson Mandela. **PICHA: MTANDAO**

## Mafua yaahirisha mechi ya Simba

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), imetangaza kuahirisha mchezo namba 69 wa Ligi Kuu kati ya Kagera Sugar dhidi ya Simba uliotarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera jana baada ya baadhi ya wachezaji kuonekana kuwa na dalili za mafua na kukohoa, imeelezwa.

Tayari kikosi cha Simba kilikuwa kimeshatua Bukoba kwa ajili ya maandalizi ya mchezo huo wa raundi ya nane.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya TPLB ilisema kuwa mechi hiyo sasa imeahirishwa na itapangwa tena siku nyingine kuzingatia kanuni ya 34:1 (1.3) na ya 34.2.

Taarifa hiyo ilisema ni baada ya wachezaji 16 wa Simba kuonekana kuwa na dalili za mafua na kukohoa, hali iliyochangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa.

**“Sababu ya kuahirisha mchezo huo ni taarifa ya kitatibu kuwa wachezaji 16 wa Simba kati ya 22 waliosafiri kwenda Bukoba wameonekana kuwa na dalilia za mafua na kukohoa, hali iliyochangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa kama ilivyowahi kutokea miaka ya nyuma,” ilisema sehemu ya taarifa hiyo.**

Juzi baada ya kufika Bukoba, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema robo tatu ya wachezaji wa timu hiyo walikuwa wakikabiliwa na homa, kikohozi na mafua.

Mapema jana, Matola alisema kabla ya kusafiri kuelekea Bukoba, wachezaji na viongozi wote walifanya vipimo na majibu waliyopata yamesababisha kupelekea kuahirishwa kwa mchezo huo.

“Hali ya wachezaji si nzuri, ni hatari kama tungelazimishwa kucheza, ni vyema kujali afya na maisha ya wachezaji wetu,” alisema Matola ambaye naye pia ni mgonjwa.

Simba yenye pointi 18 ndio mabingwa watetezi na katika msimamo wa ligi hiyo inashika nafasi ya pili, vinara ni Yanga ambao wana pointi 20 kibindoni.

9 770856 541002 >